# Mungu Wa Wakati Huu Mwovu

Jeffersonville, Indiana USA
Agosti 01, 1965A

1 [Ndugu Orman Neville anasema, "Ripoti hii, baada ya mkutano wa pamoja wa shemasi na halmashauri ya wadhamini ya maskani ya Ijumaa usiku, tunasoma maazimio haya ambayo yatamhusu kila mwanamume, kila mwanamke, ambaye ni mfuasi aliyeidhinishwa wa huduma hii, ambaye angetaka kujua nia ya halmashauri, mchungaji na mchungaji mssaidizi. Nilisoma maazimio haya asubuhi ya leo. Kila mtu alisikilize kwa makini na kwa usikivu awezavyo." Ndugu Neville anasoma maazimio yafuatayo — Mh.]

["Maazimio haya yalifanywa na kupitishwa na halmashauri ya wadhamini, na mashemasi wakikubaliana kabisa na mchungaji na mchungaji msaidizi.]

["Kanda zote za mahubiri ya Kasisi William Branham zinapaswa kutengenezwa na Fred Sothmann peke yake, mpaka hapo halmashauri itokapo eleza vinginevyo. Hatutambui wakati huu huduma yoyote ya kanda ya bure. Kanda hizi zina haki, na haziwezi kuchapishwa tena na mtu mwingine yeyote zaidi ya Fred Sothmann isipokuwa kwa ruhusa yake yamaandishi.]

["Namba mbili. Hakuna mtu anayefanya mikutano, anayeuza vitabu ama kanda, kuandika vipeperushi, kutoa vitambaa vya maombi au kadi za namna yo yote, ama kuomba karama yo yote, asiyejulikana na kanisa hili wala mchungaji wake. Wanafanya jambo hili chini ya udanganyifu, na hawajapewa mamlaka ya kufanya hivyo.]

["Tatu. Kanisa hili halitumi wahudumu wowote mbali na mchungaji wake, Kasisi William Branham, kufanya ibada mahali pengine.]

["Sababu za maazimio haya ni kama ifuatavyo: ]

["Imefahamishwa kwetu ya kwamba wahudumu wanazunguka nchi wakiingia katika makusanyiko mengine, wakisema wanashirikiana nao, na wanatumwa na kanisa hili kufanya mikutano hii.]

["Pia tumejulishwa kwamba watu wanachapisha kadi na vipeperushi, wakituma vitambaa vya maombi na kadhalika, kana kwamba wameruhusiwa kufanya hivyo na kanisa hili na mchungaji wake, jambo ambalo si kweli. Itathaminiwa kama utalijulisha kanisa juu ya mtu yeyote atakayekutwa akifanya hivi.]

["Maazimio haya yamesomwa na kuidhinishwa na mchungaji Kasisi William Branham, mchungaji msaidizi Kasisi Orman Neville, na wadhamini na halmashauri ya mashemasi."]

[Ndugu Neville basi anasema, "Bwana na awabariki." Katika ibada ya jioni, 65-0801E, Ndugu Branham anaelezea jinsi halmashauri ya kanisa ilivyofanya maamuzi haya. Sehemu tupu kwenye kanda.]

Mambo yatendeka, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, tu …

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

Mpendwa Baba wa mbinguni, tunashukuru asubuhi ya leo kwamba tunaweza kuamini. Imewezekana kwa Damu iliyomwagika ya Mwanao, Yesu, kwamba tupate kuwa washiriki wa neema Yake; na tufanywe wana na binti za Mungu, kwa kutii Kwake hata kufa msalabani, tuhesabiwe haki kwa kumwamini Yeye na kufufuka Kwake, na sasa Roho Mtakatifu amemwagwa mioyoni mwetu.

2 Tunashukuru kwa ajili ya nafasi hii ya kuja hapa asubuhi ya leo kushiriki mawazo yetu na kuabudu kwetu, kujieleza kwa nyimbo, shuhuda, kusoma Zaburi, kusoma Neno Lako, na kumngojea Roho Mtakatifu kwa uchaji kutuletea Ujumbe uliokusudiwa kwa ajili ya saa hii. Tujalie, Bwana. Jalia tufaidike kwa kuwa hapa leo. Na tutakapoondoka kwenye jengo hili, na tuseme kama wale waliotoka Emau, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi asubuhi ya leo?" Tujalie mambo haya, Mungu wa Milele, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ketini.

Habari za asubuhi, marafiki, hapa, hapa nje katika maskani na kwa marafiki zetu kote nchini, kote kutoka Pwani ya Magharibi, tena asubuhi ya leo, hadi Pwani ya Mashariki, na kaskazini na kusini, kwenye mawasiliano ya simu.

Ni siku nzuri hapa Indiana, kidogo, yenye mawingu kidogo, baridi, nzuri sana. Maskani yamejaa, huko nje na kuzunguka kuta. Tuko chini ya matarajio makubwa kwa Bwana kututembelea leo. Nasi tunatumaini ya kwamba Mungu amekupa siku njema popote ulipo. Nayo ni siku njema, kwa kuwa Bwana ameitoa. Haidhuru hali ya hewa ikoje, ni siku nzuri. Tuna furaha kuwa hapa, bado tuna furaha kwamba tuna nafasi ya kuuelezea ulimwengu imani yetu katika Yesu Kristo. Nasi tunataka kuchukua kila nafasi tuwezayo kuchukua kuonyesha matendo yote ya upendo Wake na yale aliyotufanyia. Leo tuna …

3 Nilipewa, muda mchache uliopita, tangazo la—la kutangaza, halafu nina mambo machache hapa

ningetaka kusema. Na mmoja wapo, nilipewa tangazo kuhusu mkutano wa halmashauri usiku wa juzi. Na kumekuwa na shemasi mmoja kutoka kanisani ambaye amehamia Arizona, ambaye ni Ndugu Collins, ndugu yetu mpendwa. Na wakati akiwa hayuko, wao, halmashauri, imemchagua Ndugu Charlie Cox kuchukua mahali pake wakati yeye ameondoka. Na Ndugu Charlie Cox amechaguliwa rasmi na wadhamini…ama halmashauri ya mashemasi ya kanisa hili, kuchukua kazi ya Ndugu Collins, wakati hayupo.

4 Na jambo ninalotaka kusema, tena, ninataka kuwashukuru ninyi nyote, maana wengine wenu huenda wakaenda nyumbani kabla ya ibada ya uponyi usiku wa leo, kwa ajili ya vizawadi vidogo vizuri, upendo. Tumeletewa chakula kingi tangu tumekuwa hapa. Na kutoka kwangu na mke wangu, na familia yangu, hakika tunafurahia jambo hilo. Wakati mwingine mimi husahau hata kusema chochote juu ya jambo hilo. Nina shughuli nyingi sana, mwajua. Akili yangu iko katika mzunguko wakati wote. Mnaweza kuwazia ni kitu gani, juu ya watu, si kutoka tu kutoka papa hapa kwenye kanisa hili, bali kutoka kila mahali duniani. Mnaona? Na kwa namna fulani jambo hilo linakuweka daima katika fadhaa

Mtu fulani alikuwa akisema juu ya kuwekwa wakfu kwa watoto wachanga, na ibada za ubatizo, na kadhalika. Hilo ni zuri sana. Laiti ningaliweza kufanya jambo hilo, lakini linatatiza sana, ni—ni vigumu kwangu kupata wakati. Sina budi kuweka akili yangu moja kwa moja kwenye huu, Ujumbe huu. Mnajua Biblia iliwaambia mitume, ama … Mnajua Biblia iliwaambia wale mitume, ama…Wale mitume, hasa, katika Biblia, walisema, "Nendeni makatafute, miongoni mwenu, watu wenye sifa njema, na watu waaminifu na waliojazwa na Roho Mtakatifu, ili kwamba wayashughulikie hayo mambo." Nami nikamwambia Billy …

Yeye alisema, "Unaenda kumweka wakfu yule mtoto mchanga wakati huu, baba?"

Nikasema, "Loo, jamani!" Mnaona? Kama … Tuna wengi wao wanaongojea kuwekwa wakfu, na hiyo ni kweli, itanibidi tu kurudi na kuchukua siku maalum kwa ajili ya kuwaweka wakfu watoto wachanga. Kwa hiyo ningetaka kufanya jambo hilo, sasa.

5 Lakini tunataka kumshukuru kila mmoja wenu kutoka mioyoni mwetu; mke wangu, mimi, na familia yetu. Watu wanatuletea vyakula vya makopo, maharagwe mabichi, matikiti maji, matikiti, loo, maforsadi. Kila kitu tu kinachoweza kuwaziwa, wanakileta.

Ndugu fulani wa thamani na dada yake, juzijuzi, walituletea bata mzinga mnene. Ningali ninamla. Na kwa hiyo tu … Na kwa hiyo ninii tu…Loo, nami sina budi kummaliza kabla sijaondoka, nadhani. Kwa hiyo kama simmalizi, mke wangu atambeba twende naye. Na kwa hiyo—kwa hiyo tutaninii … Hakika sisi tunathamini mambo haya. Ninawajua watu wengi; baadhi yao siwajui. Wao watakuwa wamekaa ukumbini tutakapoingia. Na kwa hiyo hakika ninathamini jambo hilo.

Na wengi ninawajua. Nina … Nimewaona wengi, na kuna wengi ambao siwaoni. Ni—nina hakika ya kwamba kila mtu anafahamu ya kwamba ni—ningetaka kumfikia kila mmoja kama ningeweza, bali mimi ni mmoja tu. Mnaona? Ku … Siwezi kumfikia kila mtu. Ninafanya kila kitu ninachojua namna ya kukifanya.

6 Kwa hiyo, Mungu awe pamoja nanyi. Nina hakika ya kwamba kuna Mmoja ambaye atakuwa pamoja nanyi; huyo ni Yesu Kristo, Naye anaweza kuwa. Yeye ndiye Mtu pekee aliye kila mahali. Na Yeye pia ni mwenye nguvu zote, ili aweze kutimiza kila haja. Na, anayejua yote, pia anajua mahitaji yako, yale unayohitaji.

Ninamwamuru kila mtu kwamba sitaninii … Nimekuwa nikifanya haraka niwezavyo, hata tangu nimekuwa hapa asubuhi ya leo, nami nitamfikia kila niwezaye kumfikia. Na kama … Jambo ninalokosa, Mungu aliye mwenye nguvu zote ata—atawapeni kila mnachotaka kadiri ya utajiri Wake katika Utukufu.

[Ndugu Branham anatulia, kisha anazungumza na Ndugu Neville — Mh.] Siwezi kusoma huo vizuri sana. Mtausoma?

Ni tangazo maalum la namna fulani. Nami nafikiri Billy Paul hana budi aliliandika. Kwa hiyo yeye ni kama mimi; Hata siwezi kusoma maandishi yangu mwenyewe. Na kwa hiyo nina mwandiko wangu mwenyewe wa mkato. Na kama mngaliona baadhi ya maandiko yangu hapa, yaliyoandikwa hapa, mnafikiri mngaliyaelewa hayo? [Ndugu Branham anaonyesha kusanyiko lake andiko, naye anacheka pamoja nao — Mh.] Nina kitu kama nyota, inavuka daraja, na kadhalika, yote tu.

[Ndugu Neville anasoma tangazo — Mh.]

Ndugu Adair, Adair wa Arkansas, kumwona Kasisi Pearry Green nyuma ya kanisa mara moja. Vema.

7 Sasa, kwa hiyo jambo lingine ambalo ninge—ningetaka kutangaza hapa ni—ni kwamba, usiku wa leo sasa kwa ajili ya ibada za uponyaji. Tutawaombea wagonjwa usiku wa leo, na kwa hiyo na—natumaini ya kwamba mtakuwa hapa.

Nasi tunatuma salamu kwa watu wote kote nchini, katika Jina la Bwana Yesu, kwamba Mungu atawabariki asubuhi ya leo. Wengine wenu wanakaribia saa sita. Huko New York, ni karibu saa sita. Na huko Arizona, Pwani ya Magharibi, ni kama saa saba tu. Kwa hiyo kuna … Na hapa tuko moja kwa moja

katikati. Kwa hiyo Mungu akubariki unaposikiliza. Sasa hii huenda ikawa …

Nimeyachukua moyoni mwangu, nilipokuwa hapa …

8 Na hatukuruhusiwa kukodisha jumba la mikutano, na hatimaye kwa namna fulani wakaturuhusu; tungeweza kufanya ibada moja, ila hatupaswi kuwaombea wagonjwa. Si—sininii … Hiyo ndiyo huduma yangu. Sina budi kufanya yale Roho Mtakatifu ananiambia nifanye. Kwa hiyo ni—nilikataa jambo hilo, kwa sababu ninataka kuwa huru kufanya lo lote Roho Mtakatifu asemalo kufanya. Mnaona? Kwa hiyo nilifikiri tunaweza tu kuteseka siku moja zaidi, hata hivyo, katika maskani. Na ni baridi asubuhi ya leo. Bwana ametufanyia tu siku njema hapa, kwa hiyo tunashukuru.

9 Sasa, katika kufanya jambo hili, nimekuja hapa kwa kusudi la kufundisha vile Vitasa vya mwisho, vile Vitasa Saba vya mwisho, na zile Baragumu Saba za mwisho, na zile Ngurumo Saba za mwisho, za Kitabu cha Ufunuo, kuziunganisha pamoja katika wakati huu ambao tunaishi sasa; kufuata kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba, zile Nyakati Saba za Kanisa. Kwa hiyo, tusingeweza kupata nafasi ya kufanya jambo hilo. Kwa hiyo na—natumaini ya kwamba, mara niwezavyo, tutaninii … tunaweza kupata mahali pa kutosha kwa ajili ya jambo hilo, ama hapa au Louisville, New Albany, ama aidha kuweka hema, ili tuweze kukaa tu mradi Bwana anatuongoza kufanya hivyo.

Lakini katika jambo hili sasa, nilichukua nafasi hii kuwaeleza watu imani yangu na imani yangu kwa Mungu, na kisha kuwaleta kwenye saa tunayoishi. Na kwa jambo hili, halielekezwi kwa mtu ye yote yule, kanuni za imani, cho chote kile; ni kama tu ninavyoona Neno la Mungu. Na Jumapili iliyopita tulikuwa na kumwagwa vizuri sana kwa Roho juu ya Neno. Ulikuwa mrefu sana, nami nilichukia kukaa muda huo wote; lakini hata hivyo hatujui ni wakati gani tutakaokutana kwa mara yetu ya mwisho. Nasi hatuna budi, kama … tunataka kuwa. Ninataka kuwa, hasa, kama Paulo wa zamani alivyosema, "Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya Kusudi lote la Mungu." Yesu alisema hakuwaficha kitu wanafunzi Wake.

Na kwa kuwa mimi, ninashughulika sana na kujaribu kukaa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, kuona ninii—ile saa, Ujumbe wa wakati huu ni nini, wakati mwingine ninashindwa kutoka na kufanya majukumu yangu kama mtumishi wa Kristo, kama mhudumu. Lakini nina watu kadhaa wanaojaribu kunisaidia kufanya jambo hili, nami ninashukuru kwa ajili hiyo, ndugu zangu wote wahudumu.

10 Sasa, simaanishi kujaribu kuwaweka watu. Kama ninyi, huko nje nchini ambako Ujumbe unaenda, mngeweza kusimama na kuangalia kila mahali humu kanisani asubuhi ya leo, kwenye marefu ya kanisa, vyumba vya watoto wachanga, huko nje, redio zimefunguliwa, kwenye mabasi, matrela, na kadhalika, na motokaa, mngeweza kuona shida ni nini. Halafu basi kila ibada, wengi, wengi wakipita kwa magari; wakipiga simu, na kadhalika, hawangeweza kuja, karibu na hapa. Nasi tunahitaji nafasi zaidi ili watu waweze kuketi na kustarehe.

Halafu kuleta U—Ujumbe ambao ninafikiri ni muhimu sana, najisikia kwamba inatupasa, kila mmoja, tujisikie vizuri tukiwa tumeketi, ili kwamba tuweze kusikiliza; tukiwa na penseli zetu na karatasi, na mihitasari na Biblia, na kadhalika, kuandika mi—mihitasari. Lakini kwa njia hii nilifikiri ningerudi nyuma kwenye wakati tulio nao, tunaoishi, na kujaribu kuleta baadhi ya mambo haya ambayo mtakabiliana nayo. Nawe utayahitaji.

11 Kama nikija hapa leo, ama siku yo yote ile, ama mhudumu mwingine ye yote, kujaribu kuleta ujumbe kwa watu, watu wanaokufa kama sisi, na wakati umekaribia sana, kama ninavyoamini kwa siku hii; ningekuwa mnafiki kujaribu kuleta kitu ambacho ninajua ya kwamba mngekifurahia na kingekuwa dhidi ya Neno la Mungu, ama kitu fulani kuvutia umati wa watu, ama—ama kitu kama hicho; ni—nisingekuwa… nisingekuwa kile ni—nilicho hapa kuwa, mtumishi wa Kristo. Ninataka kuleta kitu fulani ambacho nafikiri ni muhimu sana kwenu, si kwa ajili tu ya kuonekana; bali kufikiri ni kitu ambacho kama nikifa leo, kesho kitatiwa nanga moyoni mwako kuendelea na kumtumikia Mungu.

12 Sasa nataka kusema ya kwamba kuna jambo fulani linalojiandaa kutukia. Ninajua jambo hilo. Wengi wenu hapa mnakumbuka wakati Ndugu Junior Jackson aliponijia kidogo kabla ya kuelekea Arizona, juu ya ndoto aliyokuwa nayo. Jambo la ajabu! Ni wangapi wanaokumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Naye Bwana akatupa fasiri yake, nalo likatukia kikamilifu. Sasa, yeye ameota tu ndoto nyingine, kitu fulani.

Na jambo la ajabu, mtu fulani alikuwa hapa juzijuzi, kutoka Oregon. Ni vigumu kwake kunijua, naye alikuwa… aliota ndoto ile ile juzijuzi, ambayo Junior Jackson aliota, na—na akaja akaniambia. Si—sijui tafsiri yake; Ninamngojea Bwana. Lakini ninajua itakuwa kitu fulani kutoka kwa Mungu. Kumbuka tu jambo hilo. Ni HIVI BWANA ASEMA. Ni kitu kinachotoka kwa Mungu. Sijui ni kitu gani. Ni ajabu kweli, ajabu sana! Kwa kweli, kulingana na—na ndoto ambazo watu wote … Mmoja wao ninge … huenda akawa ni Mbaptisti, Mpresbiteri. Hu—huenda akawa ameketi hapa asubuhi ya leo. Sijui. Alikuwa hapa hivi majuzi. Simjui mtu huyo.

Lakini yeye aliisimulia ile ndoto, huku machozi yakimtoka. Nayo ikamtikisa. Alikuja kutoka Oregon

hapa, kueleza jambo hilo. Ndugu Jackson alikuja vivyo hivyo, asubuhi ya leo. Mtu mmoja akiwa hamjui mwingine; mmoja, maelfu ya maili kutoka kwa mwingine, na ndoto zote mbili juu ya kitu kile kile kabisa. Kwa hiyo Roho Mtakatifu anaishikilia fasiri yake nisiijue. Sijui nimwambie mtu huyo nini. Lakini ninajua Mungu anajitayarisha kufanya jambo fulani, nalo litakuwa tukufu machoni petu.

13 Sasa, Ujumbe asubuhi ya leo, ninataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Wagalatia. Mimi sihubiri wala si … Ni somo la shule ya Jumapili. Na sasa, ninyi wanaume na wanawake mnaosimama kando ya kuta, na mtu fulani anataka kubadilishana na kuwaacha mkae kidogo, ama cho chote kile, sasa, hamtanisumbua; iweni tu na kicho. Na iwapo akina mama, watoto wao wanalia ama cho chote kile, mtu fulani atatoka kwenye chumba cha watoto wachanga ili kwamba wapate nafasi kwa ajili ya huyo mtoto mchanga.

Na sasa chukua penseli yako, Biblia, na uwe tayari kuchukua baadhi ya Maandiko ambayo tutasoma. Sitaki ujisikie umefungwa. Ninawatakeni mjisikie—ninawatakeni mjisikie huru kuketi na kusoma. Na huenda msikubaliane, jambo ambalo ni sawa. Lakini ninazungumza jambo hili kote nchini asubuhi ya leo, ili kwamba watu ambao wameamini Ujumbe ambao Bwana Yesu amenipa kwa ajili ya saa hii, wapate kujua yanayotendeka, na kuyaweka katika Maandiko.

14 Jumapili iliyopita tulizungumza juu ya *Watiwa Mafuta Katika Siku ya Mwisho*. Na kama wewe, ye yote wenu, ni wasikilizaji wa kanda, hakikisheni mnapata kanda hiyo. Si kwamba tunataka kuuza kanda; hilo silo wazo. Nia ni kuupeleka Ujumbe nje. Mnaona? Mnaona? Kama una mashine ya kucheza kanda, kusanya kundi la watu pamoja, ukaicheze, na msikilize kwa makini. "Watiwa Mafuta." "Watiwa mafuta."

Mnawasikia watu wakiinuka na kusema, "Loo! Biblia ilisema, 'Katika siku za mwisho, manabii wa uongo watainuka na kufanya ishara hizi.'" Hayo ni Maandiko hasa. Basi hayo yanatumika mahali gani? Halina budi kutumiwa vizuri.

Usiku wa leo ninataka kuzungumza juu ya, Bwana akipenda, juu ya: *Mungu Akifunuliwa Katika Neno Lake Mwenyewe*, namna ambavyo jicho haliwezi kutumika mahali sikio linapopaswa kutumiwa. Mnaona? Ni kama tu kuchapisha Biblia nzima, na, katika Biblia nzima, inamwonyesha Yesu Kristo. Kwa hiyo ninataka kuzungumza juu ya jambo hilo usiku wa leo, Bwana akipenda. Na sasa, kama sivyo, tarehe fulani ya baadaye.

15 Sasa katika Kitabu cha Wagalatia. Na katika Kitabu cha 2 Wakorintho 4:1 hadi 6, kisha Wagalatia 1:1 hadi 4, ninataka kusoma Maandiko. Sasa katika Wagalatia 1:1 hadi 4, "Paulo, mtume," angalia kule kusimama upesi sana. Mtume maana yake ni "mmoja aliyetumwa," ama, "mmishenari."

> *Paulo, mtume, (si mtume wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali ... na Yesu Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu),*
>
> *Na ndugu wote walio pamoja nami, kwa makanisa ya Galatia;*
>
> *Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo.*
>
> *Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu ... Baba yetu.*
>
> *Utukufu una Yeye milele na milele. Amina.*

16 Sasa katika Kitabu cha Wakorintho wa Pili, mlango wa 4, nasi tutasoma aya ya 1 hadi 6, aya.

> *Kwa sababu hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivyopata rehema, hatulegei;*
>
> *Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu.*
>
> *Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea;*

Kama hiyo haileti kuchaguliwa tangu zamani, sijui ni kitu gani kinacholeta.

> *Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu.*

Kama ilivyokuwa katika Bustani ya Edeni, "Wafukuze, wasije wakagusa ule Mti."

> *Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; ... na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu.*
>
> *Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo.*

17 Amina! Hivyo ndivyo Neno linavyosomeka! Sasa, somo langu asubuhi ya leo, ni: *Mungu Wa Wakati Huu Mwovu.* Kama tulivyosoma katika Maandiko, "mungu wa ulimwengu huu, wakati huu mwovu." Sasa, Ujumbe huu unaonyesha uovu wa wakati huu mwovu, na unafaa kwa unabii kwa ajili ya wakati huu mwovu.

Na ninaamini kwamba kila … ya kwamba Biblia ina kila jibu kwa kila wakati, tayari limeandikwa katika Biblia, kwa ajili ya mwamini wa wakati huo. Ninaamini ya kwamba kila kitu tunachohitaji kimeandikwa papa Hapa, kinahitaji tu kufasiriwa na Roho Mtakatifu. Siamini ya kwamba mtu ye yote duniani ana haki ya kuweka tafsiri yake mwenyewe kwenye Neno. Mungu hahitaji mtu ye yote kufasiri Neno Lake. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Yeye alisema angefanya jambo hilo, Naye hulifanya.

Kama nilivyosema mara nyingi. Yeye alisema, "Bikira atachukua mimba," Yeye alisema hayo kwa midomo ya nabii, naye akachukua. Hakuna mtu anayepaswa kufasiri jambo hilo. Hapo mwanzo, Yeye alisema, "Iwe nuru," na ikawa. Hakuna mtu anayepaswa kulifasiri. Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, Yeye angemwaga Roho Wake juu ya wote wenye mwili," Naye akamwaga. Sihitaji mfasiri wa ye yote wa jambo Hilo. Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, mambo haya" (ambayo tunaona yakitendeka sasa) "yatakuwa hapa." Haihitaji tafsiri yo yote. Tayari limefasiriwa. Mnaona?

18 Sasa, angalia kwa makini sasa tunapojifunza Neno. *Mungu wa Wakati Huu Mwovu,* tunaoishi sasa. Huenda likaonekana ni la ajabu, jambo la ajabu sana, katika wakati huu wa neema, wakati, "Mungu anawachukua watu kwa ajili ya Jina Lake," huyo ni Bibi-arusi Wake, katika wakati huu mwovu ambao unapaswa kuitwa wakati wa uovu. Wakati ule ule ambapo "Mungu anawaita watu kwa ajili ya Jina Lake," kwa neema, kutoka, na unaitwa wakati mwovu. Sasa, tutathibitisha kwa Biblia ya kwamba huu ndio wakati aliokuwa akinena habari zake. Ni jambo la ajabu sana kuwazia hilo, ya kwamba katika wakati mwovu kama huu, ya kwamba Mungu wakati huo angekuwa anamwita Bibi-arusi Wake.

Mnaona, Yeye alisema, "watu," si "kanisa." Kwa nini? Hata hivyo, linaitwa Kanisa, bali Yeye angewaita "watu." Sasa, kanisa ni mkusanyiko wa watu wengi wa namna mbalimbali. Lakini Mungu anamwita mmoja hapa … Yeye hakusema, "Nitaita Methodisti, Baptisti, Pentekoste." Yeye alisema angewaita watu. Kwa nini? Jina Lake. Mnaona, watu; mmoja kutoka Methodisti, mmoja kutoka Baptisti, mmoja kutoka Lutheran, mmoja kutoka Katoliki. Mnaona?

Lakini Yeye anawaita, si kundi la kanisa, bali "watu kwa ajili ya Jina Lake," wanaopokea Jina Lake, wanaohusika katika Jina Lake, wanaoenda kwenye arusi kuolewa Naye, wapate kuwa sehemu Yake, mnaona, kwa kuchaguliwa tangu asili. Kama tu vile mwanamume anayechagua mke mzuri maishani, aliyechaguliwa kuwa sehemu ya mwili wake. Kwa hiyo, hiyo ni kusema, Bibi-arusi wa Kristo atakuwa, na sasa, tangu zamani, amechaguliwa na Mungu kuwa sehemu ya Mwili huo. Mnaona? Loo, Maandiko ni tajiri sana, yamejaa asali!

19 Angalia, si kile mtu fulani amesema, wala mtu fulani alioita; bali ni wale waliochaguliwa na Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, naye anawaita watu hawa katika siku za mwisho; si madhehebu. "Watu kwa ajili ya Jina Lake." Na wakati huu mwovu ni wakati ambapo Yeye anafanya jambo hilo, wakati huu huu wa udanganyifu.

Juma lililopita, katika Mathayo 24, ulikuwa ndio wakati wa udanganyifu sana wa nyakati zote. Nyakati zote za udanganyifu, tangu bustani ya Edeni, kote kote, hapajakuwako na wakati wa udanganyifu kama huu. "Manabii wa uongo watatokea na kuonyesha ishara na maajabu, ikiwezekana kuwadanganya walio Wateule." Mnaona? Sasa, ni makanisa baridi tu, ya kawaida, yaliyo magumu, na kadhalika, ya theolojia ya kujibunia, hayo hayangeweza; Wateule wasingejali jambo hilo kamwe. Lakini ni kule juu karibu sana na jambo lililo halisi. Kuacha tu Neno moja ndivyo tu unavyopaswa kufanya. Ameahidiwa wakati; wakati mkuu sana! Enyi Wakristo, kila mahali, jihadharini na saa tunayoishi! Andikeni, na msome, na msikilize kwa makini.

20 Ni kwa nini Mungu angewaita watu kwenye wakati huu mwovu, kwa ajili ya Jina Lake? Sababu yake ni, ni kumjaribu, Bibi-arusi Wake. Ni ku … Wakati Yeye amedhihirishwa, akajaribiwa, kuthibitishwa, akathibitishwa kwa Shetani. Kama vile ilivyokuwa hapo mwanzo, ndivyo itakavyokuwa mwishoni.

Wakati mbegu inapoanza ardhini, inachipuka kupitia kwa wabebaji, uhai wake, bali inaishia kwenye mbegu ile ile kama ilivyokuwa wakati ilipoingia ardhini.

Na vivyo hivyo mbegu ya udanganyifu ilipoanguka ardhini, katika Edeni, ndivyo inavyoishia katika siku za mwisho.

Kama tu vile Injili ilivyokuwa wakati ilipoangukia kwenye dhehebu huko Nikea, Rumi, inaishia katika dhehebu la hali ya juu.

Kama tu vile Mbegu ya Kanisa ilivyoanguka huko nyuma, ikiwa na ishara, maajabu, na Kristo aliye hai miongoni mwao, inaishia katika siku za mwisho chini ya huduma ya Malaki 4, na kuirudisha tena Imani asili iliyotolewa mara moja.

21 Tunaona sasa, wakati huu mwovu ni kuthibitisha, kwa Shetani, Yeye si kama Hawa, ya kwamba Yeye si mwanamke wa aina hiyo. Naye atajaribiwa kwa Neno Lake, Bibi-arusi, kama vile bibi-arusi wa Adamu alivyojaribiwa kwa Neno. Na bibi-arusi wa Adamu aliamini kila sehemu ya Neno, lote, ila akachanganyikiwa kwenye ahadi moja, ya kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," leo; Lakini akashindwa kwenye ahadi moja, kwa kujaribiwa na adui, uso kwa uso. Na sasa, watu wanaoitwa kwa ajili ya Jina Lake, bila shaka, ni Bibi-arusi Wake. Yeye atakutana tena na jambo lile lile; si kwa kweli tu ya kimadhehebu ama kitu fulani, bali kila Neno!

Kwa kuwa, katika mwanzo wa Biblia, mwanadamu alipewa Neno la Mungu apate kuishi kwalo. Neno moja, likafasiriwa vibaya na m—mtu aliyeitwa Shetani, katika utu wa mnyama aliyeitwa nyoka. Shetani, katika mtu huyu, angeweza kuzungumza na Hawa, na kumfasiria vibaya Neno, kisha akapotea. Mnaona, halina budi kuwa ni kila Neno.

22 Katikati ya Biblia, Yesu alikuja na kusema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno," wakati alipojaribiwa na Shetani.

Sasa, Mungu akituambia hapa katika siku za mwisho, ya kwamba, "Mungu wa ulimwengu huu atainuka katika siku za mwisho."

"Na ye yote atakayeongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima."

Mungu na aturehemu! Na tusitembee kama wenye majivuno, vifua mbele, kichwa juu, wajuvi, kwa maana sisi pia wakati mmoja tulikuwa katika kuasi. Hebu na kwa neema, na rehema, na kujisikia moyoni mwetu kwa Mungu, kwa unyenyekevu tuje kwenye Kiti cha Enzi cha neema.

Ajabu sasa, baada ya yapata miaka elfu moja mia tisa ya kuhubiriwa kwa Injili, na sasa yeye, huo ni mfumo wa ulimwengu, ni mwovu zaidi kuliko katika siku ambazo, wakati Yeye alipokuwa hapa. Mfumo wa ulimwengu ni mwovu zaidi. Ulimwengu unaelekea kwenye kilele kikuu. Mnajua jambo hilo. Bwana anatimiza Neno Lake kwa kila njia.

23 Jana, nikisimama … Natumaini mdogo jamaa hataninii … Hatafanya hivyo. Nilikuwa nimekuja na mke wangu, na Bibi Woods, Ndugu Roy Roberson, mahali fulani hapa, Ndugu Woods, tulikuwa tumesimama hapa kwenye Kituo hiki cha Maduka ya Youngstown, kuchukua ki—kifurushi alichokuwa nacho Dada Woods. Na kwenye … tulipokuwa tumesimama pale, jamaa mmoja mdogo akaja na kujitambulisha, na si mgeni kwangu. Kijana mwingine alikuja na kusema walikuwa wanatoka ama Alabama, Georgia- … Ninaamini Georgia, maana niliwauliza kama walimjua Ndugu yetu Welch Evans. Nasi tulizungumza kwa dakika chache. Na wakati nilipoanza kuodoka, huyu kijana mdogo alinitazama. Wakati huyo jamaa mwingine mdogo na mvulana wake mdogo walipokuwa wakiondoka, huyu kijana aliniangalia. Akasema, "Jambo moja tu nataka kusema."

Nikasema, "Je! Wewe—wewe ni mwamini? Wewe ni Mkristo?"

Kasema, "La, bwana." Akasema, "Nime- …"

24 Huenda nisinukuu neno alilosema hapa, lakini huenda alikuwa kidogo anatilia shaka. Nilikuwa nimemuliza kuhusu kule kutokea kwa Malaika wa Bwana. Naye alisema alikuwa amesikia habari zake, bali hakuwahi kwenda kanisani hapo kabla, kanisa hili. Nikasema, "Je! Unaamini?"

Kasema, "Naam, bwana." Akasema, "Ni—nimekuwa nikiangalia kitu fulani." Kasema, "Watu wamekuwa wakiniambia kuhusu utabiri huu na kadhalika, nami nikasikia kwenye kanda kwamba umebashiri jinsi California itakavyopasuka namna hiyo." Kisha akasema, "Nilipoona jambo hilo kwenye gazeti, ndipo nikaamini." Yeye alisema, "Ninakuja leo ama kesho," hiyo ni leo, "kwa mara yangu ya kwanza."

Nikasema, "Bwana akubariki, mwanangu," kisha nikaanza kumpa mkono.

Akasema, "Lakini ninataka kukwambia jambo fulani, bwana." Yeye alisema, "Nimepotea namna kupotea kuwezavyo kuwa." Akasema, "Mimi ni kama sarafu kwenye lundo la mchanga, nimepotea!"

Nikasema, "Lakini haikubidi kukaa hivyo. Kuna Mtu fulani anayesimama hapa sasa ambaye anaweza kukupata wakati wo wote ambapo upo tayari kupatikana."

Akasema, "Niko tayari."

Nikasema, "Waweza kuinamisha kichwa chako?"

Akasema, "Sioni haya."

Si hilo tu, bali alipiga magoti, pale kwenye maegesho, mbele ya watu wote. Watu barabarani wakimwangalia. Hapo tukaomba pamoja naye, mpaka akampa Mungu moyo wake. Alikuja, akiwa mwenye dhambi; akarudi, mwana wa Mungu. Alienda karibu na motokaa, amekufa; akarudi, akiwa hai.

Nikasema, "Kidimbwi kitafunguliwa kesho."

Kuna chemchemi iliyojaa Damu,
Imetolewa kwenye vena za Imanueli,
Ambapo wenye dhambi walitumbukia chini ya gharika,
Hupoteza hatia yote.

Nikasema, "Simama ukabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, ukiliitia Jina la Bwana. Mungu atakujaza na Roho Mtakatifu, na kukupa mambo haya makuu, na kukufanya upate kuyaona."

25 Ni kitu gani? Ulimwengu unaelekea kwenye kilele. Kwa nini? Roho ya uasi, upotovu wa maadili, dini ya kisayansi, imeiongoza kwenye "ngome ya kila ndege wenye chuki na wachafu," kama Biblia ilivyosema. Hebu na tusome jambo hilo, Ufunuo 18. Wakati tu tunapoanza jambo hili, tunapata Ufunuo 18:1 hadi 5. Nafikiri nimeweka hilo sawa.

> *Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake.*
>
> *Akalia kwa sauti kuu,* (enyi watu mlio na zile ndoto) *... akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, ... na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;*
>
> *Kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake* (kanisa), *na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake.*
>
> *Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, ... wala msipokee mapigo yake.*
>
> *Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.*

26 Ni onyo lililoje! Hilo linalitupa kanisa kabisa kwenye Ufunuo 3:14, kwenye wakati wa Laodikia, uasi; wa kidini halisi, bali ni waasi. "Wewe, kwa sababu unasema ya kwamba, 'Sisi ni matajiri, hatuna haja na kitu,' wala hujui ya kwamba wewe ni uchi, mwenye mashaka, kipofu, wala hujui." Linganifu kabisa na Maandiko ya wakati huu, si kwa Maandiko ya wakati wa Danieli, si kwa ya wale katika jina la…wakati wa Nuhu, lakini katika wakati huu wa mwisho, mwovu.

Angalia hapa, "U uchi." Hebu hilo lilowe kabisa kabisa. Ninajua huenda nisiwe na kutokubaliana sana juu ya wazo hili, lakini imefikia mahali ambapo ni vigumu kwa Mkristo kutoka nyumbani mwake na asiletwe mbele ya wakati huu mwovu, na wanawake wasiovalia vya kutosha.

27 Enyi wanawake, nitasema jambo hili, nami nawatakeni msikilize. Na, wanaume na wanawake, huenda msikubaliane na jambo hili, lakini ninajisikia kuongozwa kulisema. Je! Ulijua, mwanamke ye yote anayejivua nguo hivyo hana akili timamu? Je! mnajua, yeye ni, aamini asiamini, ama hafikirii hivyo, yeye ni kahaba? Ingawa mwanamke huyo anaweza kusimama ameweka mkono wake mbele za Mungu na kuapa ya kwamba yeye hajaguswa na mwanamume mwingine ye yote ila mumewe, na hiyo inaweza kuwa ni kweli kabisa, bali hata hivyo yeye ni kahaba. Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye." Na mwanamke huyo anaweza kuwa …

Mnaona, yeye ni "uchi," Biblia ilisema, "wala hajui." Roho inayomtia mafuta kufanya mambo kama hayo ni roho mwovu, roho ya kikahaba. Utu wake wa nje, mwili wake, nyama zake, huenda akawa msafi. Huenda asifanye uzinzi wo wote, na angeweza kumwapia Mungu na kuwa kweli, ya kwamba kamwe, bali roho yake ni roho ya kikahaba. Yeye amepofushwa sana na mungu wa ulimwengu huu wa mitindo; alijivalisha kimapenzi na akatoka akaenda kule.

28 Hivi majuzi, mimi na Ndugu Wood tulikuwa tunaweka mtumbwi wetu mtoni. Ilibidi niondoke nyumbani kwa dakika chache, niende mtoni. Na po pote ulipokwenda, wanawake wakiwa na makundi haya madogo ya … yanayoitwa 'kinis ama kitu kama hicho, karibu nao. Hiyo ni fedheha. Mwanamke hawezi kuwa na akili timamu na kuvaa kitu kama hicho. Amepagawa na roho ya kikahaba. Sasa, tengeneza hilo kwa Mungu, mama, maana utaona siku moja ya kwamba hiyo ni Kweli.

Ungewezaje, bibi, ukijua jinsi mwili wako ulivyo wa heshima sana, na kuuanika kule nje kwa haya mashetani yenye tamaa mbaya na yenye dhambi yanayotembea kwenye mitaa ya siku hizi? Kama wana wa Mungu wote wangalikuwa bado ni wana wa Mungu, mumeo alikuwa mwana wa Mungu, aidha angekufanya uvae nguo ama akuache. Kama mvulana alikuwa mwana wa Mungu, kamwe asingeoa kitu kama hicho. Mnaona?

Unasema, "Wewe una- …" La.

Ninawaambia Kweli, na siku moja mtakutana Nalo. "Uchi, mzinzi; hujui."

"Loo, naapa ya kwamba sikuvunja nadhiri za mume wangu." Mume wako atakuhukumu kwa jambo hilo kama ulifanya hivyo. Lakini Mungu atakuhukumu ni roho wa aina gani aliye ndani yako; si kukuhukumu kwa mwili wako, bali kwa roho yako, mtu huyo wa ndani.

29 Mtu wa nje ni kiumbe chenye mwili ambacho kinatawaliwa na hisi sita … ama hisi tano, hasa. Mtu wa ndani ni mtu wa roho ambaye anatawaliwa na hisi tano; dhamiri, na upendo, na kadhalika. Mtu wa nje; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia.

Lakini ndani ya roho hiyo ni nafsi, na inatawaliwa na jambo moja, hiari yako. Unaweza kukubali yale ibilisi anayosema ama kukubali yale Mungu asemayo. Na hiyo itaamua ni roho gani iliyo mle ndani. Kama ni Roho wa Mungu, atakula mambo ya Mungu, wala hatakula chochote cha ulimwengu. Yesu alisema, "Ukiipenda dunia au mambo yaliyo katika dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakujaingia kwenye sehemu hii ya ndani." Shetani amekudanganya. "Na mwanadamu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Angalia sasa, tunaona ya kwamba yeye ni "uchi," mchafu na uchi.

30 Na ulimwengu unaonekana kuwa katika wakati mwovu sana uliopata kuwa. Kamwe katika wakati wo wote wanawake hawakutenda namna hiyo, kamwe ila kabla tu ya kuangamizwa kwa ulimwengu uliotangulia gharika. Naye Yesu alirejea kwenye jambo hilo. Tutalifikia hilo baada ya kitambo kidogo.

Je! Mungu amepoteza mamlaka, ama anaruhusu tu mamlaka nyingine itawale? Nashangaa. Jibu la kweli la swali hili ni, kwa maoni yangu, kuna roho mbili zinazopingana ulimwenguni leo, zinazotenda kazi. Sasa, hakuwezi kuwa na zaidi ya viwili, vichwa viwili. Na mmoja wao ni Roho Mtakatifu akitenda kazi; huyo nyingine ni roho ya ibilisi, na, katika siku hizi za mwisho, katika udanganyifu.

Sasa nitaweka msingi wa mawazo yangu papa hapa kwa ajili ya somo lililosalia, yale mengine … Ujumbe wetu.

31 Zile roho mbili. Mmoja wao, Roho Mtakatifu wa Mungu; huyo mwingine, roho wa Ibilisi, akitenda kazi katika udanganyifu. Watu wa dunia sasa wanafanya chaguo lao.

Roho Mtakatifu yupo hapa akimwita Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo. Yeye anafanya jambo hilo kwa kuthibitisha Neno Lake la ahadi Kwake, kwa ajili ya wakati huu, akionyesha ya kwamba ni Kristo.

Kama kidole kinapaswa kusogea katika wakati huu, kidole kitasogea. Kama mguu unapaswa kusogea katika wakati huu, mguu utasogea. Kama jicho linapaswa kuona katika wakati huu, jicho litaona. Mnaona?

Roho wa Mungu, wakati anapokuwa akafikia kimo kikamilifu cha Mungu, ndio wakati tunaoishi sasa. Roho Mtakatifu yuko hapa akithibitisha Ujumbe wa wakati huu. Naye Roho Mtakatifu anafanya jambo hili, ili kwamba watu wanaomwamini Mungu wataitwa watoke kwenye machafuko haya.

Roho mchafu wa Ibilisi yuko hapa akiliita kanisa lake kwa upotovu, kama kawaida, kwa kupotosha Neno la Mungu, kama alivyofanya hapo mwanzo. Angalieni likirudi moja kwa moja kweye wakati ule wa mbegu tena; kutoka Edeni, hii hapa tena. Hii hapa tena.

32 Sasa, kurudi kule nyuma, wewe ni wa…nyakati zingine, ulikuwa mfuasi wa madhehebu, ulikuwa mfuasi wa *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Ni nini kilichotukia kwa ule ubua wa kimadhehebu? Unakauka. Roho anaendelea kuondoka na kuendelea, na inaelekea katika Mbegu. Mnaona?

Na jaribio, la wote wawili, linarudi nyuma namna lilivyokuwa hapo mwanzo. Angalia. Usi—usininii, la, usisahau jambo hilo sasa.

Kama vile Yohana, Yohana wa Kwanza 4:5 na 6, ukitaka kuliandika, yeye anaandika, "roho ya upotevu."

Hawa kamwe hakutoka tu, kirahisi, akasema, "Simwamini Mungu." La. Ilikuwa ni upotevu alioamini.

Shetani kamwe hakuja na kusema, "Loo, vema, hilo hata si Neno la Mungu." Yeye alikubali ilikuwa ni Neno la Mungu, bali aliweka tafsiri yake mwenyewe Kwake. Ambapo, Mungu aliwaambia waziwazi wasifanye hivyo.

Hili linafanya nini? "Linaleta nguvu za upotevu, watu wauamini uongo, na wahukumiwe nao." Sasa kama ukitaka kusoma hayo, Wathesalonike wa Pili 2:11.

Kama nilivyo nayo kadhaa, Maandiko machache hapa, na hatutaweza kuyasoma yote. Moja sasa na kisha, nitawapeni ninyi. Kama linavyoonekana ni jambo la ajabu, kwamba unahoji jambo hilo ama kitu fulani, nasi huenda tukaandika na kusoma kwa—kwa manufaa yako.

33 "Kuleta nguvu za upotevu," kama Biblia ilivyosema ingefanya, Wathesalonike wa Pili. "Sasa, mtu huyu

wa kuasi angetokea, na kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kwamba alikuwa Mungu, na kuwafanya watu waingie katika nguvu za upotevu, wauamini uongo; na, wauamini, watahukumiwa nao."

Hilo ndilo jambo lile lile alilomfanyia Hawa. Mpe … Kamwe—kamwe hakumwambia Neno halikuwa kweli, bali alimpa nguvu za upotevu, hata akauamini uongo.

Roho ya udanganyifu ni ya ibilisi. "Mashetani sasa wanafanya kazi katika wana wa kuasi." Kuasi nini? Wana wa siku hizi wanaasi nini? Kama vile Hawa alivyokuwa, hapo mwanzo, Neno la kweli la Mungu. Hiyo ni kweli. Sasa kama ungetaka kupata hilo …

Hebu na tulifungue, Waefeso 2, kwa dakika moja, maana inaonekana ni vizuri kwamba sisi … Nitasimama kwa dakika moja tu, kama hamna haraka sana, na kusoma baadhi ya haya. Waefeso 2:1 hadi 2.

*Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;*

*Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi;*

34 "Wana wa kuasi." Na kama mpinga Kristo, akianza kule katika utoto wa kuasi, itakuwaje wakati atakapoishia katika utu wa mpinga-Kristo? Namna itakavyokuwa danganyifu! Ni udanganyifu wenye nguvu zaidi jinsi gani mtu—mtu mzima anaweza kuutolea ulimwengu, kuliko wa mtoto mchanga! Naye akasema, "Roho ya—ya upotevu sasa inafanya kazi katika wana wa kuasi," wasiotii Neno. Angalia. Sasa nataka kukaa kwenye jambo hili kwa dakika moja, "wana wa kuasi," mtoto.

Hivi ulijua, wewe, mwanzo wako, ninaweza kuthibitisha kwa Neno la Mungu ya kwamba wewe, mtu ye yote aliye humu ndani, ulikuwa hai katika babu wa baba yako. Na babu wa baba yako, ulizaliwa kupitia kwa babu, halafu baba yako, halafu wewe. Mnajua jambo hilo?

Biblia ilisema, ninaamini ni Waebrania 7, ya kwamba, Melkizedeki, Ibrahimu aliporudi kutoka kuwapiga wafalme, "Ibrahimu alimpa Melkizedeki sehemu ya kumi ya nyara zote." Na huyu hapa Paulo anasema sasa, ya kwamba, "Lawi, aliyepokea sehemu ya kumi, alikuwa … Alitoa fungu la kumi, kwa kuwa alikuwa bado katika viuno vya Ibrahimu alipokutana na Melkizedeki." Kwa hiyo cho chote kile Ibrahimu alichofanya, basi tunaona ya kwamba Lawi wakati huo alikuwa ndani ya Ibrahimu, ambaye alikuwa ni babu wa babu yake. Ibrahimu akamzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo aliwazaa wale wazee wetu, Lawi.

Sasa, basi, mnaona, hapa panaonekana dhahiri, kuchaguliwa tangu zamani.

35 Sasa, katika Jumbe hizi, ninataka ku—ku—kutilia mkazo mambo niliyowaambia katika Ujumbe, wa Nuru hii ya jioni ambayo Mungu alisema ingekuja duniani.

Pia angalieni, basi, "Mnyama aliyekuwa aje duniani, angewadanganya wote ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia."

Katika mawazo ya Mungu mwenyewe; Mungu, Roho mkuu. Hapo mwanzo, kabla hapajakuwepo na mwanzo, Yeye alikuwa ni Mungu, na hivi ulijua ulikuwa ndani Yake wakati huo? Kama wewe ni Mkristo sasa, ulikuwa ndani Yake wakati huo.

Halafu basi, kama hivyo ndivyo ilivyo, Uungu wote kwa jinsi ya mwili umeumbika katika Utu wa Yesu Kristo. Na ndipo Yesu alipokufa msalabani, nilikufa pamoja Naye, kwa kuwa nilikuwa ndani Yake wakati huo; kwa kuwa Yeye alikuwa utimilifu wa Neno, lililodhihirishwa, tukijua ya kwamba tungedhihirishwa baadaye. Nasi tulikuwa pale Kalvari pamoja Naye. Tulienda kaburini pamoja Naye. Nasi tulifufuka pamoja Naye na kufufuka Kwake. Na sasa tumepanda, kwa Roho Wake, kwenye Kiti cha Enzi cha neema, tukiketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. Daima!

36 Kwa kuwa kama vile chembechembe ya maisha ya kawaida ilivyoshushwa, ikapata uhai kutoka kwa baba, kuingia kwa kwa baba, kuingia kwa baba, kuingia kwa baba, vivyo hivyo ndivyo Uzima wa Kristo ulivyo hai.

Hiyo ndiyo sababu Mungu anamtumia Roho wa Eliya mara tano mbalimbali. Ni kitu gani? Ni kupokezana.

Kama tu vile maisha yako ya kawaida na tabia zimetolewa kutoka kwa uzazi wa kawaida wa baba yako, vivyo hivyo na Roho wa Mungu, aliyechaguliwa tangu asili kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Na wakati Neno lote la Mungu, kwa ukamilifu, lilipoongozwa katika mwili wa kibinadamu unaoitwa Yesu Kristo, mle ndani Mungu alinifanya nilipie dhambi zangu, ndani Yake mle. Ndipo akanifufua,

akanifufua pamoja Naye, katika ufufuo. Na sasa tumeketi pamoja Naye, tukiwa na nguvu na mamlaka juu ya kila pepo. Loo, laiti ungaliweza tu kuamini kile Mungu ametoa! Lakini kama hujaketi pale, huna kitu hicho. Na kama umeketi pale, wala huamini, na unaogopa kusogea, hutakitumia kamwe. Lakini kama umeketi pale, utakitumia, kwa kuwa umechaguliwa kufanya kile unachofanya.

"Farao," ule upande mwingine, "aliinuliwa awe Farao kwa kusudi hili," Biblia ilisema. "Yuda Iskariote aliinuliwa kuwa mwana wa upotevu."

Sasa angalia Kweli hizi kuu ambazo tunazikaribia.

37 Sasa tunaona ya kwamba kanisa lilikataa kukubali Neno la Mungu lilitawale, na badala yake likamkubali Baraba. Sasa, kama unataka Maandiko juu ya jambo hilo, ni Mathayo 27:15 hadi 23. Hili lilifanya nini? Hili lilifanya kazi mahali gani? Sasa wazia jambo hilo. Wakati kanisa la ulimwengu, katika maisha yake ya utaratibu wa mtu mwenye haki, mtakatifu, kama walivyodhani walikuwa, na walikuwa hivyo katika macho ya watu, wao walimsulubisha Yesu, na kusema, "Hatutaki Mtu huyu atutawale." Naye Yesu alikuwa utimilifu wa Neno la Mungu. Yohana wa Kwanza 1, inaeleza jambo hilo. Nao wakasema, "Hatutakuwa na Neno hili la Mungu litutawale" Hata hivyo, Yeye alikuwa ni Neno, bali macho yao yalipofushwa kwa kile alichokuwa. Kwa kuwa Yeye alikuwa jibu la moja kwa moja kwa kila unabii uliokuwa utimie ndani Yake.

Sasa, sote tunaamini jambo hilo, kwa sababu tunaangalia nyuma kuona jambo hilo likitukia. Lakini kama ulimwengu ungeweza, huu uliopo sasa, wakati huu mwovu wa sasa, ambao ungalikuwa kule nyuma wakati ule, wao wangefanya jambo lile lile wanalofanya leo, kwa sababu lingali ni Neno lile lile, kwa ajili ya wakati huu, likidhihirishwa. Wao watafanya jambo hilo. Yeye atafanya hivyo. Hawawezi kufanya kitu kingine. "Wao ni watoto wa kuasi." "Wamepewa nguvu za upotovu, kuamini uongo, na wahukumiwe nao."

38 Angalia wakati ulimwengu wa kanisa usingemkubali Yesu, Neno, lililodhihirishwa la siku hiyo, kwa sababu (kwa nini?) Walikuwa wamelifasiri kwa njia nyingine. Lakini walipaswa kujua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye hilo Neno, kwa sababu kila kitu ambacho Mungu alisema angefanya, Yeye alikifanya. Naye akawaambia, "Yachunguzeni Maandiko ya wakati huu; na kama sitimizi masharti ambayo yalinenwa niyatimize, basi msiniamini."

Wakasema, "Tunamwamini Musa."

Yeye alisema, "Kama mngalimwamini Musa, mngaliniamini Mimi, kwa maana Musa alinena habari Zangu." Na bado hawakuliona. Mungu yule yule wa Mbinguni akifa msalabani, na kusema maneno yale yale nabii aliyosema angesema, na bado hawakuliona. Mnaona?

Hawakuwa wa aina Yake. Hawakuwa Neno, hawakuwa Neno; nao, hata hivyo, walikuwa—walikuwa wa kidini sana. Bali hawakuwa Neno, kwa kuwa Hilo—lingetambua mahali Pake kwa ajili ya saa hiyo.

39 Angalia jinsi Maandiko yanavyopatana vizuri katika kila wakati. Angalia sasa.

Na wakati ulimwengu wa kanisa haungekuwa na Neno la Mungu kuwatawala, walimkubali muuaji, Baraba. Hili lilifanya nini? Lilimkuza Shetani, mungu wa wakati huu mwovu, kufikia mahali ambapo alipataka daima.

Sasa sikilizeni. Kwa kuwa, Shetani hasemwi kama mungu wa wakati mwingine wowote ila wakati huu. Yeye hakunenwa kama mungu wa wakati wa Nuhu. Hakunenwa kama—kama mungu wa wakati wa Musa, mungu wa wakati wa Eliya. Lakini, wakati huu mwovu, yeye ndiye … Loo, usilikose! Yeye ni mungu wa wakati huu mwovu, anayeabudiwa na mamilioni na mabilioni ya watu, nao hawajui. Lakini hebu na tuache Maandiko yamfunue asubuhi ya leo, na hebu tuone, ndipo utajua. Hebu Maandiko …

Kama ilivyo katika mikutano ya upambanuzi, wakati Roho Mtakatifu anapoingia miongoni mwa Neno Lake na anamwita mwanamume huyu na kusema, "Hufai kuishi na mwanamke huyu mwingine. Ulifanya hivyo kwa nini, miaka kumi iliyopita, ulipokimbia na mke wa mtu huyo?" Yeye anafanya nini? Kumfunua, kumfunua Shetani, ambaye amemfunga mwanamume, ama mwanamke anayeishi na mume wa mwanamke mwingine, ama dhambi ambazo wamefanya, mambo ambayo wamefanya. Linafanya nini? Linamfunua.

40 Madaktari wanachukua vyombo na kujaribu kuona kuna nini. Hawawezi kufanya hivyo. Hatuwezi kueleza. Lakini basi Roho Mtakatifu anatoka na kufunua kile alicho, na kumfunua. Mnaona? Hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo. Ni Nuru inayoangaza gizani.

Na wakati unapopeleka kelele fulani chumbani, inasikika ya kisiri-siri; dude fulani linapiga makelele, wala hujui ni nini. Washa taa, upesi … Nyenje, mende, wao—wao ni wana wa gizani. Na wakati nuru inapowaka, wao hutawanyika.

"Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wa kwetu," Biblia ilisema. Mnaona? Hawawezi kuishi katika Nuru ya ulimwengu … Kwa kuwa, Mungu wa Mbinguni ametuma Nuru Yake katika siku hizi za mwisho, apate kuangaza njia kwa ajili ya watoto Wake, kusudi wasitembee katika giza na kujikwaa, bali wapate

kutembea katika Nuru ya kuangaza kwa Yesu Kristo, Yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina!

41 Angalia, Shetani hakuitwa mungu wa wakati mwingine wowote ila wakati huu. Ilikuwa ni shauku yake kuwa kama Mungu, tangu mwanzo kabisa.

Hebu na tusome jambo hilo. Tutachukua tu wakati wetu. Hebu na turudi kwenye … Mnaona, nimeandika, Isaya 14. Hebu na turudi nyuma kwenye Isaya 14, kwa dakika moja tu, tuone yale Mungu aliyosema. "Mungu," yale aliyofanya Shetani. Isaya 14:12 na 14. Angalia.

> *Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa!*
>
> *Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini.*

Ilikuwa ni shauku ya Shetani kuabudiwa kama Mungu. Alichukua theluthi mbili, theluthi mbili za nyota za Mbinguni. Alipanda juu ya nyota hizo, na kuwahubiri, na kuwadanganya theluthi mbili za hizo. Mnaona jambo hilo? Vema. Angalia, hiyo ndiyo tamaa yake.

Na sasa yeye yuko tayari, pamoja na bibi-arusi wake aliyechaguliwa kwa makini, aliyeelimika kwa maarifa yake mwenyewe, mnaona, amejipamba katika udanganyifu wake, wa majengo makubwa na madhehebu makubwa, na rangi za maarifa na theolojia, na mwenye akili na elimu, na elimu, kuudanganya ulimwengu mzima, na kuwa "mungu." Hivyo ndivyo alivyofanya. Wote wakielekea katika utu wa mpinga-Kristo, ambaye tayari ametiwa taji "halifa wa Mungu," na bibi-arusi wake wa kisayansi, anayependa mambo ya kilimwengu, wote wamevalia fahari ya elimu ya kiakili, ya kidini. Yeye amefanywa wa kidini kama yeye, na kwa tafsiri yake mwenyewe ya Neno la Mungu kama alivyomfanyia Hawa, na kama vile mwanawe Kaini alivyofanya.

Sasa mlisema, "Ati Mwana wa Shetani?"

42 Nionyeshe mahali pamoja katika Biblia ambapo Kaini aliwahi kuitwa mwana wa Adamu. Biblia ilisema yeye alikuwa "mwana wa yule mwovu," uzao wa nyoka. La, kifuniko kimeondolewa sasa, ndugu. Piramidi imefunguliwa, kama vile ufunuo ulivyoonyesha.

Angalia kile atakachofanya, mawazo yake. Alifikiri Mungu aliishi katika uzuri wa kilimwengu. Alifanya hivyo Mbinguni. Dhambi haikuanza kamwe katika bustani ya Edeni; ilianza Mbinguni, wakati Lusifa, mwana wa asubuhi, alipojitukuza katika urembo, naye alitaka ufalme mzuri zaidi kuliko ule wa Mikaeli. Naye aliwazia ya kwamba Mungu aliishi katika uzuri.

Na mwangalie Kaini. Hakutaka dhabihu ya damu. Alishuka akaja na kutoa tunda, ama—ama mashamba ya urembo juu ya madhabahu yake. Wa kidini sana, alifanya kila kitu, kile, kama tu vile Habili alivyofanya; Alitoa dhabihu, akaanguka mbele za Mungu katika ibada, mtiifu kwa kila njia, lakini bila ufunuo wa Neno.

Nalo Neno lilikuwa, tangu mwanzo, mpango wa Mungu. Lakini Mungu alifunua, kwa ufunuo, jambo lile lile ambalo Yeye alilithibitisha na kuhakikisha ya kwamba hilo lilikuwa ni kweli. Si dini, si madhabahu, si mfuasi wa kanisa, si kutoa sadaka, si kuwa mwaminifu; bali kwa ufunuo wa Neno la Mungu. Mungu akimfunulia kile ambacho …

Mama yake hakuchukua tofaa ambalo nyoka alimpa, bali alifanya mapenzi na utu wa Shetani, katika umbo la mnyama; si mnyama atambaaye, bali mwerevu kuliko wote, mwerevu kuliko wote kondeni, mfano wa mwanadamu, kitu pekee ambacho mbegu ingechanganyikana nacho. Sasa sayansi inajaribu kumpata. Wala kamwe hawatampata, kwa sababu kila mfupa mwilini mwake umebadilishwa. Lakini Biblia inatangaza ya kwamba jambo hilo ni kweli.

43 Angalia kile jamaa huyu atakachofanya sasa. Jamaa huyu, "Ataketi katika hekalu la Mungu," yaani, kanisa, "akijifunua mwenyewe kuwa ni Mungu." Sasa kama ukitaka kusoma hilo, hilo ni Wathesalonike wa Pili 2:3 na 4, na Ufunuo 13:4, 11 na 12; ambapo walinena, wote wawili manabii, wote wawili Yohana na Paulo, juu ya kile angekuwa katika siku za mwisho. Sasa wewe soma, kwa sababu nimeandika hapa. Lakini mimi … kuokoa wakati sasa.

Siku tunayoishi inaitwa, katika Biblia, "siku ya mwanadamu," siku ya mwanadamu. Hii si siku ya Mungu. Mungu si mungu wa dunia hii; Biblia inasema Yeye sivyo. Yeye ni Mungu wa Mbinguni. Lakini hii si siku ya Mungu.

Hii ni siku ya kuchagua. Aidha, uishi kwa ajili ya siku hii, kisha ufe; mchague Mungu, upate kuishi. Naye Mungu ni Neno, nalo Neno ni Neno lililodhihirishwa kwa ajili ya wakati huu na siku hii.

44 Angalia, "siku ya mwanadamu." Kama mnataka kuandika hilo, nilikuwa nikienda kulisoma. Lakini

Wakorintho wa Kwanza 5:1-5 … Wakorintho wa Kwanza 4:1-5, samahani, Wakorintho wa Kwanza 4:1 na 5, Paulo alikuwa akinena juu ya kuhukumiwa na mwanadamu, katika siku za mwanadamu.

"Ile siku, kwa nini unaiita siku ya mwanadamu?" ungesema. Ni siku ambayo kazi za maarifa ya mwanadamu zinatukuzwa.

Angalia kile, majivuno yote ya wakomunisti, mtu fulani akijaribu kumpeleka mtu mwezini. Mungu anajaribu kumpeleka mtu fulani Mbinguni. Mnaona? Lakini angalia namna wanavyotumia mamilioni na mabilioni na matrilioni ya dola, katika jitihada za bure. Watakapofika kule, hawatapata kitu. Wana shida gani?

Sijali kuhusu mwezi. Ninataka kuupita mwezi upesi sana hata sitauona; niendelee tu kwenda juu zaidi. Ninataka kupita lile Kundi Jeupe la Nyota, niendelee, nizidi kwenda tu. Naam!

45 Na ulimwengu siku hizi unajiweka wakfu kwa maarifa yaliyokuja na Shetani. Nayo siku ya mwanadamu inatukuzwa, si na Neno la Mungu, bali na maarifa aliyo nayo.

Sasa wazia. Hebu hilo lizame ndani. Na wakati mtakapocheza kanda hii, kwenye jambo hili hapa, simameni kwa muda kidogo na kuwazia.

Kazi Zake zimeinuliwa juu ya Neno la Mungu na kazi zilizodhihirishwa; hekima ya Shetani, ambayo alimpa Hawa hapo mwanzo. Sasa sikilizeni; usikose jambo hili. Hekima ya Shetani imeinuliwa kwenye kiti cha enzi cha kuabudia, katika mwanadamu, juu ya Neno lililothibitishwa la Mungu la wakati huu. Makanisa yetu yanathibitisha jambo hilo kwa ninii zao— seminari zao, shule za kusomea, ambazo mnasoma zaidi ya Neno la Mungu linavyojua habari Zake, ndivyo wanavyodhania. Na hapo, Daktari *Fulani*, na Mwalimu *Fulani*, na Profesa *Fulani* wameinua maarifa yao wenyewe, wanayoyaita (kutoka kwa Shetani) kuwa ni kweli, juu ya ahadi ya Mungu iliyothibitishwa, iliyofanywa wazi. mbele zao. Naye mwanadamu anaikubali vizuri kabisa. Mnaona?

Mafanikio Yake ya kisayansi, akijaribu kuthibitisha Neno la Mungu kuwa uongo. Wazia tu jambo hilo. Yeye, yake, hiyo ni kusema, theolojia ya mwanadamu, huwafafanulia watu Neno la Mungu, na kulifanya lisiwe na nguvu kwa watu tena, kama alivyofanya katika wakati wa kimadhehebu wakati Yesu alipotokea duniani. Yesu alisema, "Enyi wanafiki! Ninyi, kwa mapokeo yenu," hayo ni tafsiri yao, "mmechukua Neno la Mungu na kulifanya lisiwe na nguvu kwa watu." Na hilo ndilo jambo lile lile walilofanya leo. Halina nguvu.

46 Angalia, "Wao," hao watu, "wanamwinua juu ya yote yaitwayo Mungu." Je, Wathesalonike wa Pili hawasemi wangefanya hivyo? Na mamlaka ya kanisa la kimadhehebu, watu wakiamini madhehebu hayo kuliko wanavyomwamini Mungu. Na Mungu ni Neno. Wao wataamini kanuni zao za kimadhehebu kuliko Neno, ambao "wanamwinua juu ya kila kiitwacho Mungu." Na kuna Mungu mmoja tu, na huyo ni Neno.

"Yote yaitwayo Mungu; hata yeye kama Mungu huketi katika hekalu la Mungu, akithibitisha ya kwamba yeye ni Mungu," kwa sababu amewafanya watu wamwabudu. Mungu ni Neno. Mungu ni Neno. Naye anajitukuza juu ya yote yanayoitwa Mungu. Na kuna Mungu mmoja tu, na huyo Mungu ni Neno. Mnaona? "Na yote yaitwayo Mungu," ni kwamba, mungu wa wakati huu amejiinua mwenyewe juu ya Neno la kweli, la Mungu lililothibitishwa. Hiyo ni Yohana Mtakatifu 1. Mnaona? "Juu ya yote yaitwayo Mungu, hata yeye kama Mungu huketi katika hekalu ya Mungu," akiwa na mamlaka.

Angalia, naye anasifiwa kwa jambo hilo! Loo, jalia watu, Mungu, waone udanganyifu huo! Yeye anasifiwa kwa jambo hilo, na kuaminiwa kwa uchaji na watu wa wakati huu mwovu. Sasa mnaona mungu na watumishi wake wa wakati huu mwovu?

47 Sasa hebu na tuangalie likidhihirishwa. Anasema anatengeneza ulimwengu bora zaidi kwa wao kuishi humo, kwa maarifa yake mbali na Neno la Mungu lisiloshindwa kamwe. Lakini kwa kukusanyika kwake pamoja, katika madhehebu, na kanuni za imani, na kielimu, na kisayansi, na kadhalika, yeye anafanya ulimwengu bora zaidi kwa mwanadamu kuishi, na akipuuza ahadi ya Mungu, kwamba wakati pekee ulimwengu utafaa kuishi ndani yake ni katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Mnajua, maoni yangu, yeye amefanya ulimwengu bora wa kutenda dhambi badala ya kuishi ndani yake.

Angalia. Je! Alifanya hivyo? Yeye alihalalisha dhambi. Alihalalisha unywaji wa wiski, kuvuta sigara. Na katika makanisa, walihalalisha kwamba mwanamke angeweza kuwa mfuasi wa kanisa, mwenye nywele fupi. Sasa hebu tulieni kwa muda kidogo.

48 Anaweza kuvaa kaptura, kujipaka rangi, na bado ni wa kundi lake la kidini, jambo ambalo ni kinyume kabisa na Neno la Mungu. Yeye anasema ni sawa. Mnaona maarifa yake? "Hilo lina uhusiano gani na mwanamke?" Ni sawa tu na kula tunda lililokatazwa, ama si tunda lililokatazwa, hivyo ndivyo ilivyo. Mungu alisema tusifanye hivyo, bali yeye hufanya hivyo.

Naye anamwamini, naye anampenda kwa jambo hilo. Anamchukia Mungu. Matendo yake mwenyewe yanathibitisha anafanya hivyo. Anasema anampenda, bali anampenda Shetani. Yeye anamwabudu mungu

wa mitindo, mungu wa ulimwengu, miungu wa kike wa Hollywood. Anampenda, bali analichukia Neno la kweli la Mungu, ambalo ndilo Mungu pekee wa kweli aliyeko.

Analihalalisha makanisani. "Hakuna madhara. Wanawake wetu wanaweza kufanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*." Lakini katika Uwepo wa Mungu aliye hai, hata haruhusiwi kuja, isipokuwa yeye atubu.

Anaona, yeye ni mungu wa uzuri wa kilimwengu, ndivyo alivyo. Anataka kuonekana mrembo. Naye ni mungu wa uzuri, tangu mwanzo. Yeye anaweza, na amefanikiwa kwa maarifa yake katika sayansi na vifaa, kutengeneza urembo kwa ajili yake, wakati huu wa mfano … wakati huu wa kisasa, hasa, wa uovu. Umefanywa mrembo.

49 Angalia. Ni jambo muhimu kuangalia. Hapo mwanzo, Sethi na watoto wake hawakupitia njia ya kisayansi.

Sasa tutazungumza juu ya sayansi kwa dakika chache. Kama nikisema jambo hili, si kutoa udhuru kwa ajili ya ujinga wangu; lakini, kundi la wapumbavu, kitu cho chote kitakachokana Neno la Mungu. Mnaona? Hakika.

Inastahili kuangaliwa. Angalia jambo hilo. Watoto wa Sethi kamwe hawakupitia njia ya kisayansi. Walikuwa ni wachunga mifugo wanyenyekevu, wakulima, na kadhalika.

Lakini watoto wa Kaini walifanya hivyo. Kwa nini? Wakiongozwa na baba yao, ibilisi. Kaini, akiongozwa na baba yake, ibilisi, na hawa wakiongozwa na hiyo mbegu ikishuka.

Angalia uzao wa Mungu ukishuka kupitia kila wakati, na uangalie mahali unapoelekea leo. Wakristo, Wakristo halisi, hawashughuliki sana na utafiti wa sayansi na kadhalika. La. Kwa dakika moja tu, tutaingilia jambo hilo.

Lakini wa Kaini walifanya hivyo, kufuatana na tabia ya baba yao, ibilisi, aliyejaa maarifa ya kilimwengu, urembo, na sayansi, na kadhalika. Watoto wa Kaini walikuwa wa kisayansi. Walikuwa na elimu. Walikuwa wachezaji wa muziki—vifaa vya muziki; Elvis Presley wa kisasa, baadhi ya upuzi kama huo ambao halmashauri ya shule inaruhusu utendeke hapa kwenye kichochoro hiki kila Jumamosi usiku Wajenzi wa miji, wakiwapamba wanawake kwa tamaa zao za kibinafsi, kama vile ibilisi anavyowapaka wanawake rangi, na kukata nywele zao, na kuwavalisha kaptura, na mambo kama hayo. Wao, ni kwa ajili ya tamaa zake chafu. Hilo ni dhahiri sana, bali sijui njia nyingine yo yote ya kusema jambo hilo.

50 Sasa, tunajua ya kwamba injili ya Shetani ni injili ya sayansi na maendeleo. Yeye aliihubiri huko Edeni; si Mungu; Shetani alifanya hivyo, sayansi ya maendeleo. Sayansi na maendeleo ni injili ya Shetani. Angalia mahali ambapo ametuongoza hadi leo, pamoja nayo. Mnaona?

Angalia, yeye alihubiri huko Edeni, kwa nani? Kwa bibi-arusi wa Adamu. Naye akaanguka kwa ajili yake. Alimdanganya akahoji moja ya Maneno ya Mungu. Hebu tuone kile alichoweza kusema. Hapana budi alisema, "Si jambo la kisayansi kufa, katika kanisa hili takatifu." Ama, "Utafundishwa na kuelimishwa, kutokumini kitu cha kijinga hivi kama mauti. Sijali kama Neno la Mungu lilisema jambo hilo; halina busara."

51 Loo, mwangalieni leo. "Mungu ni Mungu mwema. Uko katika kanisa Lake takatifu; mbona, huwezi kufa." Lakini Mungu alisema ungefanya hivyo, na hilo latosha. Mnamwona leo? "Loo, ni washiriki tu wa kanisa. Si kile unachofanya, ama *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*. Njoo tu kanisani na uwe mshiriki mzuri. Kukata nywele zako, huo ni upuuzi. Njoo tu kanisani na uwe mshiriki mzuri. Kukata nywele zako, huo ni upuzi. Na kuvaa kaptura, kujipodoa, na kwenda kwenye madansi, na pombe kidogo mara moja moja, haitakudhuru, mradi tu isiwe kwa hanasa. Kwa kweli, laiti ninyi watoto mngaliinywa, ili kwamba wajue kama wangeipenda ama wasingeipenda." Huyo hapo, mungu wa wakati huu, wakati huu mwovu.

"Mungu ni Mungu mwema." Nimesikia jambo hilo sana hata ninakuwa mgonjwa. Mungu pia ni Mungu wa haki. Yeye si babu mkongwe mwenye madoadoa anayeweza kusukumwa kila mahali, na wajukuu Wake hawana dhambi yo yote. Yeye ni Mungu wa haki na utakatifu. Yeye alilithibitisha katika bustani ya Edeni, kwa watoto Wake wa kwanza. Unavuka mstari huo, wa moja ya Maneno Yake, umekufa. Jambo lile lile linatumika leo.

52 Na angalia, yeye alihubiri namna hiyo ya injili ya kisayansi, ya kijamii, iliyoelimika, ya kimaendeleo kwa Hawa, naye bibi-arusi wa Adamu akaiamini. Naye amefanikiwa kumjaza yule anayejiita bibi-arusi wa Kristo, kanisa la Adamu wa Pili, kwa hoja zile zile. Hiyo ni kweli.

"Loo, si—si kwa ajili ya Mungu; Mungu ni mwema sana kufanya jambo hilo. Mbona, mradi tu unaenda kanisani. 'Kama unaamini.'" Ibilisi anaamini; si kujifanya mwamini, bali yeye kweli anaamini. Yeye hajaokoka. "'Kama unaamini.'" A-ha!

Yeye anamwambia bibi-arusi wa pili, ama Bibi-arusi wa Pili wa Adamu, kama vile alivyomwambia yule wa kwanza. Kama vile, "Sasa, uponyaji wa Kiungu, hakuna kitu kama hicho. Tunaweza kuthibitisha jambo hilo. Kamwe hapajakuwapo na kesi iliyothibitishwa." "Na ubatizo huu katika Jina la Yesu, sasa hivi

hutambui ya kwamba mimi ndimi mamlaka ya kanisa?" Yeye anasema "Tumemaliza jambo hilo huko Nikea, Rumi," wakati zile roho tatu chafu zilipotoka kwenye yule joka, manabii wa uongo, na kadhalika. "Tunaamini kuna utatu wa Miungu." Loo, kwa ajili ya wema! Hao ni makafiri kadiri wawezavyo kuwa. Usije kamwe mbele za Mungu na kitu kama hicho, kujaribu kusimama katika Uwepo Wake. "Loo, haileti tofauti yoyote kama umebatizwa katika vyeo vya 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.' Inaleta tofauti gani?"

53 Ilileta tofauti kubwa sana, mpaka Paulo alipowaamuru kundi la Wabatisti kwamba iliwabidi wabatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo kabla Roho Mtakatifu hajawajilia. Na pia ilimfanya mtume huyo kupaza sauti, na kusema, "Kama malaika akija kutoka Mbinguni na kuhubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe." Hakika, inaleta tofauti. Loo, jamani!

"Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu katika siku hizi. Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya mitume tu. Umepita. Na kitu kama manabii? Hata haijulikani. Miujiza? Hiyo si wa kisayansi. Malaki 4? Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Yohana 14:12? Loo, Yesu hakumaanisha hilo kweli. Luka 17:30? Loo, hiyo ilikuwa ni hadithi ya kufikirika tu. Mnaona, ina—inafasiriwa vibaya; haikuwa katika ile ya asili." Upuuzi kama huo!

Wakati Mungu Mwenyezi anaposhuka chini miongoni mwetu na kulithibitisha. Anaposema, ya kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," Yeye anathibitisha hilo kuwa kweli. Sijali ni nani anayesema si juu yake; Mungu hulifasiri Neno Lake Mwenyewe. Yeye alisema angefanya jambo hili katika siku za mwisho. "Kutakuwako na Nuru wakati wa jioni." Na kuna Nuru, kwa ajili ya kudhihirishwa kwa Mwana wa Mungu.

54 Jua lile lile linalochomoza mashariki ni jua lile lile linalotua magharibi. Nabii alisema, "Kutakuwako na siku ambayo haingeitwa mchana wala usiku." Ni siku yenye utusitusi, yenye mawingu, kama juu ya jua. Lakini alisema, "Wakati wa jioni itakuja Nuru tena." Mwana yule yule! Yeye ni Alfa na Omega. Mwana yule yule aliyefufuka mashariki alitabiriwa kufufuka magharibi tena, katika siku za mwisho, kabla tu siku haijaisha. Sijui jinsi wanavyolifasiri; Mungu hulifasiri Neno Lake Mwenyewe. Yeye hulithibitisha. Huu ni wakati wa jioni.

Ni huzuni, lakini yeye kweli alishawishika katika jambo hilo tena. Bibi-arusi wa Kristo alishawishika, na kuchukua maarifa ya kiakili ya mhubiri fulani wa seminari badala ya kuliamini Neno la Mungu lililo safi na lililothibitishwa.

55 Sasa wahudumu huko ng'ambo nchini po pote mlipo, huenda msikubaliane na Hili. Mimi siwaudhi. Ninajaribu tu … Ninazungumza na kundi langu mwenyewe. Ninajaribu tu … Kama mkitaka kuketi, hakika nitafurahi kwenu kulisikia. Na halafu mnalisikiliza. Mnaona? Lakini ninawaambia tu yale waliyo nayo—yale waliyoona, na kuwaonyesha hayo; Mungu akilithibitisha, ya kwamba ni kweli. Mnaona?

Hii ndiyo ile saa. Haihitaji mtu ye yote kuifasiri. Maarifa yako ya kilimwengu hayana chochote … Huenda ukawa na B.A., D.D., A.D., ama chochote kile; haimaanishi jambo moja. Mungu hulifasiri Neno Lake, Mwenyewe. Yeye aliahidi jambo hilo, na hili hapa.

Lakini kwa maarifa ya seminari, mahubiri ya kimadhehebu, "yameufanya ulimwengu wote kumshangaa yule mnyama ambaye jeraha lake la mauti liliponywa," kutoka kwa upagani hadi kuingia upapa. Mnaona mahali anakoelekea? Anaamini jambo hilo. Anaamini maarifa anayomwambia.

56 Ni kwamba, sasa angalieni, ni kwamba bibi-arusi wote wawili walioposwa waliamini maarifa ya Shetani dhidi ya Neno la Mungu. Bibi-arusi wa Adamu aliamini maarifa ya Shetani dhidi ya Neno la Mungu, naye bibi-arusi wa Kristo ameamini maarifa ya Shetani, katika wakati huu mwovu wa kiakili, dhidi ya Neno la Mungu.

Na angalia. Hawa, katika mambo ya kawaida, ambaye aliamini jambo hilo, na kutumbukiza jamii yote ya mwanadamu mautini. Bibi-arusi wa kawaida! Adamu, mtu wa kawaida wa dunia; bibi-arusi wake, kabla hajamfikia, awe mke, alitumbukiza jamii yote ya mwanadamu mautini. Kama ni la kisayansi ama la, tunakufa vivyo hivyo, maana Mungu alisema tutakufa.

Kama uko katika Edeni takatifu, ama kanisa takatifu, ama dhehebu takatifu, ama cho chote kile, utakufa siku usipoamini Neno moja la Neno la Mungu kuwa ni Kweli, wakati litakapothiirishwa na kuthibitishwa kwako. Hiyo ndiyo siku unapojitenga na Mungu. Si sentensi yote tu; Neno moja. "Ye yote atakayeongeza neno moja, ama kuondoa Moja," hiyo ndiyo siku utakayokufa.

57 Angalia, bibi-arusi wa Adamu alisababisha mauti ya kawaida kwa jamii yake, jamii ya binadamu.

Na bibi-arusi wa Adamu wa Pili, bibi-arusi aliyeposwa na Kristo, amelitumbukiza kanisa lote kwenye mauti ya kimadhehebu, apate kuchukua alama ya mnyama, kwa madhehebu makubwa ya kisayansi, ya kielimu. "Sisi ni Wabatisti. Sisi ni Wapresbiteri. Sisi ni Wapentekoste," na kadhalika. "Tuna hii, na tunamiliki mali zaidi. Sisi, tunatambuliwa na serikali. Tuko kote ulimwenguni," na mambo hayo yote. "Na aliye bora zaidi, na meya wa mji, na kadhalika, anatujia. Hata Rais anakuja kufanya misa pamoja nasi, nasi tunakuja

kwenye *hili*, *lile*, ama *lingine*." Ulimwengu mzima umetumbukia kwenye mauti ya kiroho, ya kimadhehebu; kanisa lote. Amekufa!

Unasema, "Unashughulikia maeneo mengi."

Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." "Katika siku za Lutu, ambapo watatu walitolewa Sodoma, siku ile …" Sasa tayari kuna kundi tayari limetoka, kumbukeni. "Lakini, kama ilivyokuwa wakati huo, wakati Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa." Angalia ni siku gani, angalia mahali tunapoishi!

58 Sasa yeye ameufanya ulimwengu mzima kukubali uongozi wa kisayansi wa mpango wa elimu ambao Shetani amempa chini ya jina la kanisa, uongozi wa mpango wa elimu, wa kisayansi. Ninakuonyesha wewe mungu wa ulimwengu huu.

Wakati yeye, kama Hawa, alipokuwa na kujazwa kabisa kwa Neno la Mungu mkononi mwake, angaliweza kuchukua Neno la Mungu. Lakini yeye alifanya nini kwa Hilo? Badala ya kungojea ubatizo wa Roho Mtakatifu, aliacha sayansi imthibitishie ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa tu kwa ajili ya wanafunzi.

Badala ya kuendelea na uponyaji wa Kiungu, wakati anapaswa kuwa sasa akiwafufua wafu na kufanya miujiza mikubwa; yeye amemwacha Shetani, chini ya uongozi wake wa mwanamume wa kidini, achukue Neno la Mungu na kujaribu kusema ya kwamba lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Naye ameamini jambo hilo.

59 Wakati, Biblia ilisema, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya." Yesu alisema hivyo. "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Tungali tu viumbe. "Ishara hizi zitafuatana na kila mmoja wao aaminiye." Yeye hukana kila sehemu Yake.

Anakana mambo yote ya miujiza, na aliyabadilishana na wazo la kiakili la Biblia; ambapo makasisi, na baba mtakatifu, anavyojiita, ambapo maaskofu, maaskofu wakuu, ambapo wazee wa jimbo, viongozi wakuu, na kadhalika, wameweka fasiri yao wenyewe Kwake. Naye Mungu amewaacha, waketi pale, wamekufa kama usiku wa manane.

Na jambo pekee lililobaki katika siku za mwisho ni maskini kundi la Wapentekoste wenye vifaa vya muziki wanazocheza kwa fujo, wakikimbia huku na huku sakafuni, wakinena kwa lugha na kupaza sauti, "wenye mfano wa uungu, bali wakikana Neno lake." Waambie wabatizwe katika Jina la Yesu Kristo; watakucheka waziwazi. Lakini, hiyo, Mungu anaendelea moja kwa moja kuifanya vile vile kabisa, akithibitisha Neno Lake kuwa kweli.

60 Angalia, ule mti ambao Shetani alimfanya Hawa kula, ulikuwa ni "mti wa mema na mabaya." Ulikuwa ni mti uliochanganyikana.

Sasa angalia siku tunayoishi, wakati Yeye anapomwita Bibi-arusi. Yeye ana kanisa linalodai linatenda mema, wakati ni ovu, kwa kulikana Neno. Mti uliochanganyikana. Loo, useme, "Wao—wao wana mashirika makubwa. Wao—wao—wao—wao wanasaidia jambo hili. Na Msalaba Mwekundu unakubali jambo hilo. Na shule zote, wao … Angalia hapa!"

Loo, bali kataa Neno moja tu, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya upate kufa; haidhuru jinsi ya kielimu, ni nzuri jinsi gani. Yesu alisema, "Chachu kidogo huchachusha donge zima." Sehemu moja ya chachu huharibu donge. Neno moja la Mungu, likihamishwa, linaharibu Picha nzima. Vipi kuhusu mkono wangu kuwa mahali ambapo mguu wangu unapaswa kuwa? Mnaona? Vipi kama sikio langu lilikuwa hapa chini ambapo mkono wangu unapaswa kuwa? "Chachu kidogo huchachusha donge zima."

Sema, "Unajuaje kwamba ni kweli?" Mungu hulithibitisha kuwa ni kweli. Yeye hulithibitisha. Yeye alisema jambo Hilo hapa katika Neno, kisha analithibitisha. Hivyo ndivyo tunavyojua ni kweli ama si kweli.

Kukataa tu Neno moja tu ndiko kunahitajika ili kufa. Ilileta matokeo yale yale katika wakati huu mwovu, mauti ya kiroho, kama ilivyofanya kwa mauti ya kimwili kwa jamii yote ya binadamu.

61 Angalia jinsi Shetani alivyoufikia wakati huo wa kisayansi kule nyuma, wa Nuhu, kutegemea akili zao wenyewe. A-ha! Biblia inatuambia, katika Mithali, "Msizitegemee akili zetu wenyewe." Na, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na la Mungu liwe kweli." Lakini Shetani, kwa maarifa yake, tangu mwanzo kwenye bustani ya Edeni, aliwafanya watu wazitegemee akili zao wenyewe. Na, mwajua, kupitia kazi zake kuu za Max Factor alizokuwa nazo kule nyuma, aliwapata wanawake wazuri sana hivi kwamba ilimfanya mwana wa Adamu … wana wa Mungu, hasa, kuanguka dhambini na kuwaoa. Sawa. Yeye … Wanawake walikuwa warembo sana, warembo sana.

Sasa mchukue mwanamke wa kawaida mtaani leo. Wengi wenu mmesoma hadithi hiyo; hujapata kuisikia, maana ilikuja kabla ya siku zangu. Pearl O'Brien, ni wangapi waliopata kusikia habari zake? Hakika. Alipaswa kuwa mwanamke mrembo sana ulimwenguni. Mbona, hakuna mtoto wa shule anayeingia

kwenye nyumba ya shule leo ila aliye mrembo maradufu. Kwa nini? Uzuri wa wanawake utatukia katika siku za mwisho.

Wamezikata nywele zao. Waliwaweka katika nguo ndogo za wasichana. Wanavaa kaptura, na bikini, na kila wanachoita, juu yao. Wanajipodoa, na rangi ya midomo, na mambo haya yote ya kila namna, kuwafanya kitu wasicho. Mnaona? Lakini kwa maarifa ya kisayansi wameweza kufanikisha jambo hili. Je! mnajua kuna fedha nyingi zinazotumiwa kwa vipodozi vya wanawake, kuliko ilivyo matumizi, katika Marekani, mara mbili ama tatu zaidi, katika chakula tunachokula? Thibitisha jambo hilo, hiyo ni kweli, kwa ajili ya vipodozi.

62 Angalia, "Wana wa Mungu waliwaona binti za wanadamu," si binti za Mungu, "binti za wanadamu, kwamba walikuwa warembo," na ikawafanya wana wa Mungu kuanguka katika upotovu huu. "Na wakawachukua wanawake wa aina hiyo na kuwaoa," na jambo hilo likasababisha wakati wa ukahaba, kama tu ilivyo siku hizi; kama ilivyokuwa Sodoma, kama ilivyobashiriwa itakuwa siku hizi.

Kwamba, wakati wanaume na wanawake wa siku hizi wanabadilishana wake. Kama hawamtaki mke huyu, wao—wao wanaenda huko Reno, Nevada, na kuoa; na, ama kupata talaka, huyo, na kuoa tena katika dakika kumi na tano. Na wanawake ni warembo sana hata karibu hawawezi kuzuiwa. Na ni kitu gani? Ibilisi! Mnaona Shetani angali ana uzuri? Angalia.

Angalia, hawakusamehewa dhambi kamwe. Wakati huo mzuri, wa kisayansi ulikuwa ndio wakati mwovu sana ambao Mungu aliuangamiza usoni mwa dunia; wakati huo mzuri, wa kisayansi. Yesu alisema itakuwa hivyo tena kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Hiyo ni kweli? Angalia, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu," wakati wote walipojaribu kuoa … Sasa angalia, "Wana wa Mungu waliwaoa binti wazuri wa wanadamu," na Mungu kamwe hakuwasamehe kwa jambo hilo.

63 Ni kama tu vile vile mafundisho ya Balaamu, kwamba yeye alisababisha hao wanawake warembo, wenye akili na wa kisayansi wa Moabu ku-…wakiwa na macho yao matamanifu, rangi zake na poda, manukato yake mazuri, kuwavutia wana wa Mungu; dhidi ya wanawake wao wenyewe waliofanya kazi na waliokuwa na sugu mikononi mwao, wasiojipodoa. Akawashawishi, na, "Na tuoane sisi kwa sisi, kwa sababu sisi sote ni watu wamoja." Huo ulikuwa ni uongo!

Huo ulikuwa ni uongo! Ulikuwa ni—ni uongo, na kazi nzuri ya ibilisi, kuwafanya wana wa Mungu kuoa bi—binti za wanadamu. Ulikuwa ni uongo wa ibilisi, kwa Balaamu, yule nabii wa uongo, kujaribu kutabiri dhidi ya Musa aliyejaribu kushikilia jamii hiyo pamoja; kusema, "Vema, sisi tunaamini Mungu yule yule. Tunatoa matoleo yale yale. Tuna dhabihu zile zile. Tunafanya kila kitu sawa tu."

"Watafanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Mnaona? [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Tokeni kwake, enyi watu! Huna uhusiano wo wote naye!

64 Angalia, haingewezekana kwamba Mungu angefasiri Neno Lake kwa kizazi kiovu cha Kaini. La. Mungu asingewafasiria Neno Lake. Angalia … [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Mungu, yale maarifa ya kuufanya ulimwengu uwe wa kupendeza sana na wa kisayansi na wenye dhambi, ilimbidi Yeye kuuangamiza? Hivi Mungu angefanya jambo hilo, kufanya ulimwengu wa kupendeza sana, angalia hapa, Mungu akiwafanya binti Zake warembo sana, na angewavalisha kizinifu sana, hata wanawe wangewatamani na kufanya uzinzi? Nini? Mungu afanye jambo kama hilo?

Kundi hili uchi, lililovua nguo la Walaodikia, wakimwabudu Mungu wa ulimwengu huu, kupitia elimu yao ya maadili, na elimu, na werevu, na urembo! "Tokeni kwake," Biblia ilisema, "msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake." Mungu atanyesha mvua ya mawe kutoka mbinguni siku moja, ukubwa wa ratili mia kila moja, na atamwangamiza yeye kwa kumpiga yeye na mawe; kama Neno Lake daima lilivyosema Yeye alifanya, sheria Zake.

Vema, kama Mungu alifanya jambo kama hilo, akawafunulia watu kama hao Neno Lake, Yeye angekuwa— angekuwa anavunja kusudi Lake Mwenyewe. Mungu si mpumbavu. Yeye ndiye chanzo cha hekima yote.

Kwa hiyo mnaona mahali ambapo upuuzi huo unatoka? Ulitoka kwa Shetani, na ungali ni wa Shetani. Na kanisa limeamini jambo hilo.

65 Sasa mnaona, enyi wanawake, ninajaribu niwezavyo kuwaonyesha Neno la Mungu. Biblia ilisema, "Mwanamke akikata nywele zake, anaaibisha kichwa chake," ambacho ni mumewe. Na mumewe ndiye kichwa, pamoja na Mungu, kwa hiyo anamvunjia Mungu heshima na mumewe.

Sasa hii inaonyesha ni nani aliye kiongozi wa mfumo wa kanisa la ulimwengu huu. Hiyo inaonyesha ni nani aliye kichwa chake. Ni Shetani, katika umbo la mtu mwenye nguvu sana, mtu wa maarifa, maarifa makuu. Yeye anajua zaidi ya hao wengine wote. Haidhuru Neno linasema nini, yeye—yeye ana tafsiri

yake mwenyewe Kwake, mnaona, tafsiri ya wakati huu mwovu.

66 Angalia mipango yake ya kujenga kanisa kuu la kimadhehebu, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, mnaona, dhehebu kubwa sana, ili ulimwengu wote umwabudu, yule mnyama, chini ya jina la Ukristo ulioungana. Ungetaka kusoma hayo katika Biblia? Ufunuo 13:6 na 8. Ni mnara wa kisasa wa Babeli.

Hivi hamkumbuki namna ambavyo Nimrodi, yule mnafiki, alivyojenga mnara huu mkubwa na kuifanya miji mingine yote midogo kutoa kodi kwake? Babble na Babeli ni kitu kile kile. Huo hubadilisha tu majina yake, na, namna unavyojitokeza. Ni, Rumi sasa ni Babeli. Na ulimwengu mzima unaletwa Babeli, na unaletwa na Baraza la Makanisa Ulimwenguni ambalo litafanya kila mmoja wao kuinama kwake. Nawe umechukua alama ya mnyama, bila kujua ulichokuwa ukifanya. Kwa sababu …

Lakini wale walioteuliwa watalisikia Neno na kutoka kwake.

67 Namna madhehebu yalivyo kinyume na Neno la Mungu! Yeye kamwe hakuwa na moja, hakuwahi kushughulika na moja, na kamwe hakushughulika na moja. Ninataka mwanahistoria fulani anionyeshe mahali ambapo nabii aliwahi kutoka kanisani. Nionyeshe mahali ambapo Mungu aliwahi kubariki kanisa ambalo lilikuwa … baada ya kuwa dhehebu. Liliwekwa kwenye rafu na likafa, likiwa na hekima ya akili kutoka kwa ibilisi, kwa viongozi wao, na limekataa Neno la Mungu lilipokuwa linakua kufikia kiwango kikamilifu cha Kristo. Sasa limefikia kileleni. Ni tofauti jinsi gani!

Jitengeni na huyo Hawa asiyeamini, ninyi watoto wa Nuru ya jioni!

Shetani, mungu wa wakati huu, kwa maarifa yake, akiwafanya watu kula kutoka kwenye mti wake uliochanganyikana wa mema na mabaya. Angalia, Shetani, kwa maarifa yake, akiwafanya watu wa wakati huu mwovu kula kutoka kwenye mti wake wa mema na mabaya. Yeye anasema ya kwamba anajenga ustaarabu mkubwa zaidi wa Kikristo, kwa maarifa yake ya mema na mabaya, ustaarabu mkubwa zaidi wa Kikristo.

Bali maskini Bikira wa Kristo, Neno, Kundi, Bibi-arusi, hajali maarifa yake. Yeye hujiweka, huyo, hujitenga naye. Ni nini … Sasa hebu tuzungumze juu Yake, kwa dakika moja. Anamngojea Bwana Wake na sikukuu ya Milenia ya sikukuu yake, kweli, pamoja na Bwana Arusi wa Neno, kwa kuwa Yeye ni Bibi-arusi Neno.

68 Maarifa na ustaarabu, na Ukristo wa kweli, havina uhusiano. Ustaarabu, na Ukristo wa kweli, havina uhusiano kamwe.

Ustaarabu ni kwa maarifa. Sote tunajua jambo hilo. Na maarifa yanatoka Edeni, yalilithibitisha, kwa yale aliyohubiri katika Edeni. Na maarifa husababisha mauti. Hiyo ni kweli? Ni kitu gani kilichosababisha mauti katika bustani ya Edeni? Maarifa. Lakini haiwezi kuwa ya Mungu, kwa hiyo ni ya ibilisi. Whiu, hilo lilikuwa ni zuri! Maarifa, sayansi, elimu, ndicho kizuizi kikubwa sana alichowahi kuwa nacho Mungu. Ni ya ibilisi.

Sasa nitapata barua kuhusu hilo, najua. Ninawasubiri.

Angalia utamaduni ulikotufikisha sasa. Mnaona? Angalieni yale umefanya. Tuko wapi? Tumeyategemea mambo hayo, kwa ufahamu wetu wenyewe kwa sayansi yetu.

Mnasema, "Na Mungu je! unafikiri Yeye hajui?" Loo, la.

Mungu ataanzisha aina Yake Mwenyewe ya ustaarabu duniani, wakati atakapouchukua. Huu ni ulimwengu wa Shetani; yeye ni mungu sasa wa ulimwengu wake wa maarifa ya kisayansi. Lakini Mungu ataanzisha aina Yake Mwenyewe ya ustaarabu. Hautakuwa ustaarabu kama huu. Mnakumbuka tu jambo hilo. Hautakuwa ni ustaarabu wa namna hii tulio nao leo. La, la. Itakuwa kulingana na Neno Lake na kusudi Lake. Kwa kuwa, mungu wa wakati huu mwovu ataangamizwa, pamoja na ufalme wake pamoja naye.

69 Wakati huu wa kisasa wa kupenda maarifa usingeweza kuwa na kiongozi bora kuliko yule waliye naye, Shetani, mpotoshaji wa Neno la Mungu, kama alivyoanza katika bustani ya Edeni, bali mtu wa kidini akitegemea ufahamu wake mwenyewe.

Kama nilivyosema hapo awali, Mithali 3:5, ya kwamba, "Hatupaswi kutegemea akili zetu wenyewe."

Lazima wawe na mungu, kwa kuwa wao ni wanadamu. Hata hivyo, yeye huwafanyia watakavyo. Kama ilivyokuwa binadamu, daima, binadamu wote… Tulipokuja hapa, tuliwakuta Wahindi hata wakiabudu sanamu, na jua, na kila kitu. Kama mwanadamu, hawana budi kuwa na mungu. Kwa hiyo wakati huu mkuu wa kielimu hauna budi kuwa na mungu, kwa hiyo umekuwa … Mungu wa ulimwengu huu amekuwa maarifa, madhehebu, sayansi, "wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake."

70 Angalia, mungu wao anawafanya kile tu wanachotaka. Wao wana tamaa ya mwili, na huo ndio

anaowapa. "Wanataka kuvaa bikini. Acha wavae. Mnaona? Kama wanataka kufanya *hili* ama *lile*, hebu na walifanye. Hakuna madhara ndani yake; wanaenda kanisani. Mama yao alikuwa Mmethodisti, Mbatisti, Mpentekoste, Mpresbiteri. Waacheni tu."

Huyo ni mungu wa wakati huu; mwerevu, mwenye hekima, wa kisayansi. Hilo halihitaji imani. Halihitaji kuthibitisha chochote. Tayari imethibitishwa, kwa maarifa yao. "Vema, sisi ndio kanisa kubwa kuliko yote mjini," maarifa yao. "Mchungaji wetu ana D.D., Ph.D." Mnaona, hauhitaji imani yo yote; hutegemea maarifa. Acha waishi kwa njia yo yote, mradi tu wanakuja kumwabudu kwa madhehebu yao na kanuni za imani. Kuna jicho kubwa jeusi pale, lakini liangalie.

Analicheka Neno la Mungu, akisema mambo kinyume na Neno; na kujaribu, kwa maarifa yao, kuthibitisha kisayansi ya kwamba Neno si kweli. Loo, ni wakati wa namna gani tunaoishi! Mnaona mungu wa wakati huu?

71 Angalia, lakini Mungu anangojea mpaka uovu wa hawa Waamori wa kisasa utakapojazwa. Usijali, Yeye atakuwa na Musa Wake tayari wakati huo. Kutakuwa na kutoka, siku moja, kwenye nchi ya ahadi. Musa atatokea, atakayewaita watoke, "atakayeirudisha Imani ya watoto iwarudie baba zao." Litakuja, moja ya siku hizi. Haikunini!

Mnasema, "Vema, angalia jinsi tunavyofanikiwa."

Hakika, uovu wa Waamori bado haujatimia. Utakuja, moja ya siku hizi. Acha wajiangamize wenyewe.

Ustaarabu, maarifa, hupotosha Neno la Mungu wapate kuridhisha ladha yao wenyewe. Kila dhehebu hufanya jambo lile lile. Shetani basi anahubiri injili yake mwenyewe ya maarifa katika kanisa lake mwenyewe.

72 Kuna tabaka mbili tu za watu zilizonenwa katika Agano Jipya. "Wana wa Mungu, na wana wa Ibilisi." Je! Ulijua jambo hilo? Mnataka kuandika Maandiko kwa ajili yake? 1 Yohana 3:10, kama unataka Maandiko. Ninayasoma papa hapa, nimeyaandika. Vema. Vema.

Katika Waefeso 2:2, wanaitwa, "Wana wa kuasi." Kama vile Hawa alivyokuwa, waasi wa Neno la Mungu. Wana wa kutii, na kuasi, hawana uhusiano wo wote.

Basi Bibi-arusi wa Kristo anawezaje kushiriki katika madhehebu, wakati mmoja ni siyo mtiifu na mwingine ni mtiifu? Moja lawezaje, kuwa Neno; na hilo lingine, neno lililopotoshwa? Ni vipi kahaba na mwanamke msafi wanaweza kutembea pamoja katika mapatano? Hawawezi kufanya hivyo. Hawana ushirika hata kidogo. "Tokeni kati yao!" Ni la ibilisi. Ni alama ya mnyama. Yanaelekea moja kwa moja kwake sasa; madhehebu yote. Sijali ni ya nani.

Mungu anachukua, si madhehebu, "watu kwa ajili ya Jina Lake." Madhehebu hayatapokea Kweli hizi. Itachukua mtu binafsi ambaye anaweza kumwona Mungu, kuangalia Neno Lake na kuliamini, na asiwe mfuasi madhehebu yo yote; bali amwishie Mungu, si kwa ajili ya madhehebu yake, hekima ya kiakili aliyofundisha askofu fulani ama kitu fulani kilichofundisha hilo. Hiyo ni kweli.

73 Wana wa kuasi, na wana wa utii, hawana uhusiano wo wote. Mmoja wa…ni wa siku ya Nuru; mwingine, wa usiku na giza, wakati mwovu, wakati huu mwovu wa giza, vilabu vya usiku, madansi, hata hivyo ni mshirika wa kanisa. Ni sawa kwa mungu wao. Hawana hukumu yoyote juu yake; hakuna kitu kinachowasumbua.

"Mbona, hainihukumu kukata nywele zangu," mwanamke mmoja alisema. "Halisumbui dhamira yangu." Yeye hana dhamira zaidi ya vile nyoka asivyokuwa na nyonga. Hiyo ni kweli. Bila shaka sivyo. Yeye hajui dhamiri ni nini. Imekaushwa sana hata hajui ni nini. Hiyo ni kweli.

Akitembea huku na huko, juu ya Neno la Mungu, akisema, "Mbona, huo ni upuuzi wa kale. Usiende kule; wao ni kundi tu la makelele na kupiga mayowe, hata hivyo." A-ha! Hawajui zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhottentoti asivyojua hadithi za Kimisri. Hiyo ni kweli. Ni kweli.

"Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. Kwa maana hawa ndio wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga."

"Loo, mpenzi, wewe, unapaswa kufanya *hivi*. Jamani! mpenzi, nafikiri maskini mhubiri wenu mjinga pale, kama ukininii tu… Jamani, ungeonekana mrembo katika 'kini," ama cho chote unachokiita kitu hicho. "Wewe, kama ungefanya yote *haya*, *yale*, na *mengineyo*. Mbona, sigara ndogo haitamdhuru mtu ye yote. Mimi ni mfuasi wa kanisa, nawe unajua madhehebu yetu yenaheshimiwa kama ya mtu mwingine yule." Usimwamini huyo mwongo wa kale aliyepakwa rangi. Yeye anakudanganya. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

74 Ni sawa kwa mungu wao. Loo, anafikiri hilo ni zuri sana, nao wanampenda tu kwa jambo hilo.

Jamani, watabishana nawe. Watasimama moja kwa moja na kubishana nawe juu ya jambo hilo. Mbona, hakika, Shetani alisimama moja kwa moja mbele za Yesu Kristo, Neno, na kujaribu kusema, "Imeandikwa."

Naye huyo hapo, Neno la Mungu lililothibitishwa. Yeye alisema, "Rudi nyuma Yangu, Shetani!" Tembea tu na ufanye jambo lile lile.

Ni kama vile jamaa fulani alivyoniambia wakati mmoja, kasema, "Sasa, kama unaamini ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kweli, nawe unaamini unao Huo," kasema, "sasa nipige kwa upofu." Huyo alikuwa ni mhubiri. Kasema, "Nipige kwa upofu!" Akasema, "Paulo alimpiga m—mtu kwa upofu siku moja."

Nikasema, "Bwana, ninawezaje kukupiga kipofu wakati tayari wewe ni kipofu? Ninawezaje kukuua wakati tayari umekufa?" A-ha.

Akasema, "Mimi, macho yangu ni ishirini kwa ishirini!"

Nikasema, "Sehemu yako ya kimwili; bali wewe ungali kipofu."

"Haiwezekani! Biblia haifasiri mambo. Sisi hunena mahali Biblia inaponena, na kunyamaza mahali inaponyamaza."

75 Nikasema, "Vema, wakati Eliya alipokuwa huko—huko Dothani, mnaona, kulikuja jeshi lote la Siria. Ndipo yule mtumishi akakimbia, akasema, 'Loo, baba yangu!' Kasema, 'Baba yangu,' kasema, 'Waashuri wametuzunguka.'"

"Eliya alisugua macho yake, akaamka na kusema, 'Wapo wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.'"

"Yeye alisema, 'Sioni mtu ye yote.'"

"Kasema, 'Mungu, fungua macho yake.' Sasa, yeye alikuwa kipofu. Naye akamwangalia huyo nabii mzee, na juu ya milima; ulikuwa umejaa Malaika, na magari ya Moto, na farasi wa Moto."

"Naye akatoka akaenda kule, na Biblia ilisema, 'Aliwapiga kwa upofu.' Kipofu kwa nini? Kwake. Akatoka, akasema, 'Je! Mnamtafuta Eliya?'"

"'Naam, tunamtafuta.'"

"Kasema, 'Njoo, nitakuonyesha mahali alipo.' Eliya akiwaongoza kwa Eliya. Vipofu!"

Nikasema, "Unajua nitakalokwambia? Ni vile hasa Bwana wangu alivyomwambia baba yako, 'rudi nyuma yangu.'" A-ha. A-ha.

76 Angalia, wana wa utii, na wa uasi, hawana uhusiano wo wote. Wasiotii wanamwabudu mungu wao. "Loo," wao wanasema, "tunaamini Biblia." Naam, ni mti uliochanganyikana. Mnaona, wanaongeza ulimwengu na maarifa Kwake. Mti wa Shetani, uliochanganyikana; mnaona, alichukua kutoka kwenye mti wa Shetani, mema na mabaya. "Loo, tunaamini Neno." Hakika, bali si lote. Hawa aliamini Neno, pia, lakini akamwacha—akamwacha Shetani achukue mti wake na kulipotosha kidogo. Hivyo ndivyo ilivyo.

"Ye yote atakayeongeza neno moja, ama kuondoa Neno moja Kwake." Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Angalia. Vema.

77 Wakati huu mwovu ni wa giza, hata hivyo ni wa kanisa. Mungu wao, wanampenda kwa jambo hilo, jinsi anavyowaacha wafanye. Hawana hukumu. Hakuna kitu kinachowasumbua mradi tu ni washiriki wa kanisa.

Balaamu alilifundisha kanisa jambo lile lile. "Na tuungane; sisi sote ni sawa." Ilikuwa ni hila ya mwisho. Mungu kamwe hakuwasamehe kwa kuamini uongo kama huo.

Kumbukeni, ilikuwa ni dhambi isiyosameheka, mara tatu katika Biblia, kwa mtu ye yote kuongeza neno moja la ufasiri wao wenyewe kwenye Neno la Mungu baada ya Hilo kuthibitishwa kwamba ni Kweli.

Katika bustani ya Edeni, kweli, katika bustani ya Edeni, neno moja lililoongezwa lilisababisha mauti.

Wakati Balaamu alipoongeza neno, ya kwamba, "Sisi sote ni sawa," wao, Mungu kamwe hakuwasamehe Israeli jambo hilo. Kila mmoja wao aliangamia jangwani, isipokuwa wale watatu ambao Mungu aliwatoa.

Yesu alisema, "Wao, kila mmoja wao, amekufa," hao wametengwa Milele. Wote wameangamia; hawakusamehewa kamwe. Ni dhambi isiyosameheka; kamwe hawakuwasamehe. Loo, jamani!

Ikimbieni, enyi watoto wa Nuru za jioni!

78 Ona sasa ni nani kiongozi wa wakati huu wa kisasa, wa kidini, mwovu? Ni ibilisi, akichukua ule mti wa mema na mabaya, na kuuweka huko nje, angalia, akimleta bibi-arusi wake mrembo wa kanisa kwenye baraza la ekumeni kwa ajili ya arusi. Hilo ni zuri. Kanisa lake linalovutia la kisayansi, likiwa na ma—ma—madigrii yote yanayoweza kuchukuliwa; zile Ph.D. kutoka katika kanisa la Kristo, Ph.D. kutoka la Kibatisti, Kipresbiteri, Kipentekoste, na wote. Wakiwaleta wote, pamoja na mapambo yao mazuri na makanisa makubwa, wote kwenye baraza la ekumeni, "Sisi ni mmoja." Wao hawatasamehewa jambo hilo kamwe. Madhehebu fulani, kuvaa chapa ya madhehebu, ni alama ya mnyama. Tayari tumepitia jambo hilo hapa; kufanya jambo hilo. Yakimbieni, enyi watoto, yakimbieni! Mnaona? Kanisa kubwa linalovutia likienda kwenye arusi ya ekumeni, likivaa alama yake!

Kaptura, hakika, mavazi ya kilimwengu, ya zinaa, rangi, ni wanafunzi wazuri kweli wa ibilisi, kuwanasa wana wa Mungu; kumwoza mvulana mzuri mwenye malezi mazuri kwa baa la kale kama hilo. Hiyo ni kweli. Ni ninii …

79 Ulisema, "Kukata nywele, hilo lina uhusiano gani na jambo hilo?"

Ndugu, hebu na tusimame hapa kwa dakika moja. Ninajisikia tu mtu fulani akichukizwa na jambo hilo. Huenda ilikuwa huko nje kwenye simu mahali fulani.

Sikilizeni. Nywele kwa mwanamke ni nadhiri ya Mnadhiri. Nywele kwa Samsoni ilikuwa nadhiri ya Mnadhiri. Na wakati mwanamke anapokata nywele zake, yeye—yeye hukana kabisa nadhiri yake ya Mnadhiri kwamba yeye ni Bibi-arusi wa Kristo. Kwa sababu, hapo, jambo hilo moja, anaharibu Picha nzima. Kwa usahihi! Mnadhiri ni "mtu aliyewekwa wakfu kwa kusudi fulani." Hiyo ni kweli? Samsoni alikuwa amewekwa wakfu kwa ajili ya wakati fulani kusudi fulani, kwa hiyo alikuwa na nywele ndefu. Mwanamke ambaye ni mwana wa Mungu, huziacha nywele zake zikue, kuonyesha ya kwamba amewekwa wakfu kwa kila Neno la Mungu.

Kama akikikata, sijali ni kiasi gani anacheza, anaimba, yuko kwenye kwaya, anena kwa lugha, anakimbia huku na huko, ama ana kila namna ya mashirika ya misaada, amekufa. Hiyo ni HIVI BWANA ASEMA, Neno la Mungu. Wakorintho wa Kwanza 14. Naam. Amekataa nadhiri yake ya Mnadhiri na kujiuza kwa mungu wa wakati huu wa kisasa. Yeye hufanya hivyo. Sasa, aibu kwako, mama, ama mwanamke!

Kweli ni wanasaji wa wana wa Mungu, kama ilivyokuwa. Kama Yesu alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wanawake wazuri, na wana wa Mungu wakaanza kuoa miongoni mwao, ndivyo itakavyokuwa wakati atakaporudi Mwana wa Adamu." Na mungu wao anafikiri ni maarifa ya kutukuka, na ya kuvutia, na ya kisayansi. Mtindo wa Hollywood, ulioundiwa kwenye duka lake mwenyewe, hakika, hizi zote hapa zinazobana na upuuzi, mwajua.

80 Nalo, kanisa lake, kweli linapenda jambo hilo! Loo, jamani! "Ninataka ujue, mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mchungaji wetu ana akili nzuri zaidi kuliko kusema jambo kama hilo." Hana akili za kutosha kusema mambo ambayo Mungu anasema wakati huo. Mnaona?

Yeye, kanisa, kweli linapenda sana jambo hilo. Linapenda hilo. Ni yale tu liliyotaka! Yeye hatajiunga na cho chote, ndugu, ama kuja katika cho chote kitakachombidi kutenda kama kitu tofauti na Mayezebeli hawa wa kisasa walivyo, kwa kuwa hiyo ndiyo asili iliyo ndani yake.

Unawezaje kuwa na tabia nyingine yo yote…" "Ni yupi akijisumbua aweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja?" Kama ulizaliwa uwe na urefu wa futi tano, hutakuwa na futi sita. Loo! naam, kama "mtambo wa kutanua" wa Booth-Clibborn.

81 Basi sikilizeni, enyi watu, enyi kundi la akina Ricky! Kama ulizaliwa uwe mwanaume, basi tenda kama mwanamume. Hizi nywele ndefu zinazoning'inia usoni mwako, na zimesokotwa kama mambo ya zinaa, mbona, enyi kizazi cha nyoka kilichopotoshwa! Mna nini, hata hivyo?

Mungu wangu atalihukumu taifa hili siku moja kwa moto. Yeye atalizamisha chini ya bahari. Saa ya hukumu Yake imekaribia. Ulimwengu mzima utaangamia.

Upotovu wa kidini! Upotovu wa kibinadamu; wanaume hata hawajui wao ni wa jinsia gani, wala wanawake hawajui. Wanasimama na jozi ya ovaroli ya mwanamume, ama jozi ya maskini kaptula ndogo, nguo ambazo…kila hatua yake na umbo la mwili wake, na kujiita Mkristo. Yeye hata si bibi, sembuse Mkristo. Yeye ni kahaba wa mitaani anayetumiwa na Shetani, aliyevuviwa na Shetani, kuwapeleka wana wa Mungu kuzimuni, kutimiza Neno ambalo Yesu Kristo alisema lingetukia. Sikumaanisha kusema jambo hilo, bali Yeye alilisema, hata hivyo. Mnaona mahali ambapo roho hii ya kidini inatoka? Mti uliochanganyikana.

82 Mnasema, "Hizo suruali fupi zina ubaya gani," ama vyo vyote wanavyoziita, "visukuma pedeli, ama cho chote kile?"

Biblia ilisema, ya kwamba, "Mwanamke yeyote atakayevaa vazi linalompasa mwanamume, ni chukizo

mbele za Mungu." Hiyo ni HIVI BWANA ASEMA.

Na mwanamke ambaye atakata nywele zake, huaibisha kichwa chake. Na hata si … Ni dhambi kwa mwanamke kuomba akiwa na nywele fupi, Biblia ilisema hivyo, kuomba mbele za watu huku hakufunikwa kichwa chake. Naye …

Loo, unasema, "Ninavaa kofia."

Ewe mnafiki, wafundishe hao wanawake mambo kama hayo! Wakati, Biblia ilisema, "Amepewa nywele zake kama kifuniko," si kofia ya kujitengenezea. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Mimi sihusiki; Ninawajibika tu kusema Kweli. Msiwe wasio waaminifu, kama Biblia ilivyosema, "Kulichanganya Neno la Mungu na uongo," ku—kufanya ama—ama kutimiliza matakwa ya kundi la akina riketa.

83 Nina neno *uovu* hapa. Niliandika "Elvis" badala ya *uovu*. Yote yanafanana. Neno Elvis linamaanisha "paka," na neno *Ricky* linamaanisha "panya." Unaposema "Ricky mdogo," unamaanisha, "panya mdogo." Kile mnachomwita, hivyo ndivyo alivyo. Mtoto wako anaitwa hivyo, mbadilishe upesi, kwa ajili ya Injili. Usimwite mtoto …

Hamjapata kamwe kusikia majina kama hayo huko nyuma katika Biblia, ama katika wakati mwingine wo wote. Ni wakati, jina la wakati huu. Kulikuwako na panya na paka waliopotoshwa, wako pale.

Yote haya…?…vifaa vya muziki za dola milioni moja, na hawa watoto wakitembea hapa nje, hawawezi hata kwenda—kwenda shuleni bila kidude kinachoning'inia sikioni mwao, na maskini redio ndogo mfukoni mwao, ikienda, "buum-bu-buum."

Loo, walikuja pale nyumbani, nasi tukatengeneza … Hao jamaa waliokuwa wakijaribu kupaka nyumba yangu rangi kule. Tulisema, "Ondoa kitu hicho hapa. Kama huwezi kufanya kazi bila hiyo, basi ondoka kazini. Inanifanya niwe na wasiwasi sana hata siwezi kusimama hapa. Tumeweka mahali hapa wakfu kwa Mungu. Hatutaki upuuzi wa aina hiyo wa boogie-woogie wa siku hizi za mwisho hapa." Nikasema, "Zima au uondoke kazini!"

Angalieni, wa kidini, hata hivyo, loo, hakika, wanaenda moja kwa moja kanisani na kusimama sebuleni, wakisikiliza muziki wa kipuzi.

84 Pia, angalia, Bibi-arusi Neno wa Kristo anaelekea kilele, pia. Tunapoona mahali mpinga-Kristo anakoelekea, alivyoanzia kule nyuma na sasa anafikia kwenye kilele; baraza la ekumenia litaliweka chini ya kiongozi wa kanisa. Na lile Kanisa dogo lililokuja moja kwa moja, pia, Bibi-arusi Neno wa Kristo kote katika nyakati, anafikia Kileleni, maana Yeye ataunganishwa tena na Mwenziwe. Daima, kama tu vile kanisa na cho chote kile, halina budi kuungana. Ile Ngano, cho chote kile, inavyorudi moja kwa moja kwenye kilele chake ilikoanza; kama vile Kaini na Habili. Bibi-arusi-Neno akielekea katika Utu wa Neno la Mungu lililodhihirishwa katika wakati huu mwovu tunaoishi. Mnaona mahali linapoelekea?

85 Naye Shetani hivi karibuni atamchukua bibi-arusi wake wa kielimu na kumwinua huyu mtu mkuu, ambaye ni mpinga-Kristo, ule uongozi wa kikanisa, na kumweka juu ya kiti cha enzi, "na dunia yote itamstaajabia yeye."

Na ndipo Kristo atakuja. Na mawili hayawezi kuishi katika wakati ule ule. Na ufalme wake utatwaliwa; ataangamizwa.

Naye Kristo, Neno la Mungu … Ambapo, mwanamke ni sehemu ya mwili wa mwanamume. Wao si wawili; wao ni mmoja. Na Bibi-arusi, Kanisa, Neno, "watu walioitwa kutoka *hapa* na *pale*, kwa ajili ya Jina Lake," wataungana katika Mwili wa Yesu Kristo.

Na ufalme wa mpinga-Kristo utatwaliwa na kuangamizwa. Ndipo Kristo atakitwaa kiti cha enzi, na kuketi kwenye kiti cha enzi cha baba Yake Daudi, na kutawala juu ya nchi miaka elfu moja; kisha atalikabidhi Kanisa kwa Mungu, "bila waa wala ila." Naam!

86 Sasa angalia nywele zake ndefu, nadhiri ya Mnadhiri kwa Neno. Nitamwonyesha Bibi-arusi wa Kristo sasa. Tulimwonyesha mpinga-Kristo, mahali alipo, wa dini na kadhalika, sayansi. Sasa maskini Bibi-arusi mnyenyekevu wa Kristo huamini tu Neno, hata awe nani. Ni watu binafsi. Ninatumaini na ninaamini ya kwamba kuna watu wengi wameketi hapa, wengi wanasikiliza. Nami ninatumaini ya kwamba mimi mwenyewe, na kila mmoja wenu ninyi nyote, ni sehemu ya huyo Bibi-arusi. Natumaini wengi. Na, itakuwa, wote waliochaguliwa kuwa huyo watakuwa huyo, maana ndiyo asili yao. Wao wanaona. Neno linaweza tu kulitambua Neno. Haliwezi kutambua madhehebu ama upotovu. Inajua vizuri zaidi; Ni Neno. Mnaona? Haliwezi kutambua chochote …

Ngano haiwezi kuwa kitu ila ngano. Ilianza, ngano; itaishia, ngano. Wala gugu haliwezi kuwa ngano, ingawa linatiwa maji na upako ule ule. Mnaona? Bali si ngano. Kama nilivyosema hivi majuzi, kuhusu ule mti ulio na matawi mbalimbali ndani yake.

87 Nywele zake ndefu, nadhiri ya Mnadhiri, zinaonyesha ya kwamba Yeye amemwekea Mungu nadhiri. Joho lake zuri la Neno Lake lililoahidiwa kwa ajili ya wakati ambao Yeye anaishi, aliloviringwa nalo, likimthibitisha pamoja na Yeye Mwenyewe, kwa Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa kuwa, Yeye ni sehemu ya Bwana Arusi Neno, mkweli Kwake kwa kila njia.

Sasa angalia. Kama mwanamke akitoka nje hapa naye ameolewa na mwanamume, na anatoka na kufanya mapenzi na mwanamume mwingine na anashiriki naye, na arudi kwa mumewe, huyo mume anapaswa kumfukuza. Hiyo ni kweli? Hana budi kuwa mwaminifu kwa mwanamume, maana yeye ameweka nadhiri kwake.

Na Bibi-arusi wa Kristo ameahidiwa kwa Kristo; Naye ni Neno.

Hata asikonyeze jicho upande ule mwingine, mwanamke hapaswi hata kumkonyezea jicho mwanamume mwingine. Hapaswi kufanya ishara zo zote, asionyeshe kuvutiwa ko kote naye, kwa maana yeye yakini ni bibi-arusi wa bwana-arusi mmoja.

Hatutaki hata mmoja wa miti yenu iliyochanganyikana, madhehebu yenu. Iweni waaminifu kwa Kristo, Neno. Yeye atathibitisha kwamba ni kweli. La, bwana, si hata kuvutiwa ko kote kwa cho chote kinachohusu kufanya mapenzi naye, si kujiunga na makundi yake wala cho chote kile, ama kumwacha akushike kwenye mikono yake ama kukushughulikia, ama—ama kuzungumza nawe juu ya jambo *hili*, jambo *lile.*

Unasikiliza Sauti moja tu. "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Mgeni hawatam- …" Sauti Yake ni nini? Sauti ya mtu ye yote ni neno lake. Nalo ndilo Hili, Biblia, neno moja lisiongezwe Kwake au kuondolewa Kwake. Dumu tu moja kwa moja na hiyo Sauti. "Mgeni hawatamfuata," dhehebu.

88 Kama vile, Yeye ni sehemu ya Bwana Arusi, mwaminifu Kwake katika kila jambo, akingojea Arusi. Kuungana, si kwenye baraza la ekumeni; bali hewani, kwenye Karamu ya Arusi. Yeye amepewa … Hili ni kwa ajili ya kanisa letu wenyewe. Ninii … Yeye amepewa, na zimefunuliwa Kwake, zile siri za Muhuri Saba za Biblia. Mnaona? Yeye anaona ujinga wa yule mdanganyifu, akiwa karibu sana na ile Kweli, hata karibu awapoteze walio Wateule. Yeye huliona hilo. Yeye …

Mnaona zile roho mbili zinazopingana zikifanya kazi katika wakati huu mwovu? Mnaweza kuona jambo hilo? Kila mmoja wa kidini sana, Kaini na Habili, roho tena zikija vichwani mwao, zingali vile vile zilivyoanza. Moja, ikiabudu kwa urembo, na kwa maarifa, na kwa elimu, na kwa sayansi, na kwa elimu ya maadili. Na huyo Mwingine, kwa imani ya ufunuo wa Neno la Mungu. Wote wawili wamesimama moja kwa moja katika jengo hili asubuhi ya leo. Hiyo ni kweli.

89 Ufunuo, ama imani, katika Neno Lake, havidai kuwa na maarifa; Mkristo halisi na wa kweli.

Wanasema, "Je! Una—una digrii ya udaktari?"

Hana madai yoyote. "Ni—ninaamini Neno Lake." Mnaona? Hatoi madai yoyote. Hadai kuwa na elimu. Si mfuasi wa madhehebu yo yote, chama cho chote, madhehebu yo yote. Ni mali ya Kristo. Ni Mke Wake; si mke wa kanisa.

Yeye ni kahaba. Biblia ilisema yeye alikuwa ni "kahaba," na, "MAMA WA MAKAHABA," nao wote wanakusanyika pamoja na kufanya kahaba yule yule. Na mwanamke wa namna hiyo ni mwanamke asiye mwaminifu kwa Mumewe; na kumdai Kristo kama mumewe, na ni mfuasi wa dhehebu. Upuuzi kama huo! Sisi ni mali ya Kristo.

90 Lakini, katika utii, maskini Mwanamke huyu wa imani, anayeishi kwa imani, Bibi-arusi; mtu huyo hapa, pale; hapa, ametoka mahali pengine; kanisa lingine, madhehebu mengine fulani, cho chote kile, katika ninii fulani ... Anaamini Neno la Mungu, ni mtiifu, anangojea katika upendo, kwa ajili ya kuthibitishwa kwa ahadi ya wakati huu. Yeye anangojea jambo hilo. Yeye ni sehemu ya Neno hilo, Naye anangojea uhai Wake udhihirishe hilo Neno.

Ndugu, hamwezi kuona jambo hilo? Natumaini hilo halikuwapita.

Mwili unangojea (ambao ni Neno), unangojea Uzima (ambao ni Roho) kuuthibitisha ama kuufanya hai. Hicho ndicho anachongojea. Hakuna uhai mwingine utakaofanya kazi ndani Yake. Hawezi kufufuka kwa njia nyingine. Hata hivyo, Yeye huuhisi huko nje, Naye anajua litatukia; halafu hili hapa linatukia, ndipo anaamka. Mungu alisema, "Na iwe," naye akatokea kama yule wa kwanza alivyotokea.

91 "Wana wa kuasi" maana yake ni utii … Kutotii maana yake ni "uasi." Niliangalia hilo katika kamusi, kuwa na hakika. Uasi, kuasi (nini?) Neno la Mungu lililofunuliwa. Kama vile Kaini alivyofunua … aliasi ufunuo wa Habili uliofunuliwa, uliothibitishwa na Mungu ya kwamba ulikuwa ni wa haki. Naye Kaini akaasi dhidi yake, akamwuua ndugu yake.

Mafarisayo, wakiwa na maarifa yao wenyewe ya kimadhehebu ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa

nini, watu waliochaguliwa kwa mkono, waliasi Neno la Mungu lililothibitishwa lililodhihirishwa kwa ajili ya siku hiyo, Yesu Kristo, nao wakamwua. Hiyo ni kweli?

Hivyo ndivyo "wana wa kuasi" walivyo, uasi dhidi ya Neno la Mungu.

Sasa angalia mahali walipo? "Loo, siku za miujiza zimepita. Yesu Kristo si yeye yule bado. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mambo yote hayo ni upuuzi!" Mnaona, uasi! Si lazima waseme mambo mawili; inawapasa tu kusema jambo moja, yatosha. Huo ni uasi, papo hapo. Hawawezi kusema huna macho, huna masikio; huna budi kuchukua mwili mzima, Neno lote. Mnaona?

Roho Mtakatifu anaita, "Ondokeni kwake, msishiriki mafundisho yake ya sharti ya kimadhehebu," wakati anapocheka na kudharau Neno la Mungu la siku hii.

"Kwa maana Mungu hadhihakiwi," kumbukeni tu. Yeye atakiona. Usiwe na wasiwasi. Yeye atakiona. Biblia, katika Waefeso 4:30, kama unataka kuandika hilo, Waefeso 4:30, ilisema. "Mungu hadhihakiwi. Na cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." Hawawezi kudhihaki na kufanya mzaha, na kusema mambo haya, na kujiepuka jambo hilo. "Kama mkate juu ya maji, watavuna."

92 Yeye ni bibi-arusi wa Ibilisi, amefunikwa katika maarifa yake ya kidini, yanayopenda dhambi kwa wakati huu mwovu wa sasa, kukudanganya. Loo, jamani! Kundi zima ama madhehebu ya roho zinazoshawishi, kwa maarifa ya kisayansi na ustaarabu wa kisasa! Anadai …

Tutafunga katika dakika chache tu. Itanibidi kukoma, maana siwezi kuyamaliza yote, mnaona.

Akidai ya kwamba anajenga ulimwengu mkuu kwa ajili yako upate kuishi ndani yake. Yeye anadai, ya kwamba, katika ustaarabu wake, amejenga makanisa mazuri, vyuo, shule, hospitali, maktaba, na msaada wa dharura kwa mwanadamu, bila Neno la Mungu. Amefanya jambo hilo. Amethibitisha ya kwamba angeweza kufanya hivyo. Nao watu wameanguka kwa ajili yake; naam, bwana; shule, madhehebu, utamaduni, watu waliovaa vizuri, watu waliolishwa vizuri.

Afadhali niwe kwenye mstari wa mkate, na kuwa sawa na Mungu; kuliko kuwa na kuku wa kukaanga mara tatu kwa siku, na inanibidi kuwa mfuasi wa kahaba namna hiyo.

93 Kumbukeni, saa imekaribia wakati alama itakapokuja. Ama utakuwa ndani yake ama nje yake. Itakuja kama mwizi usiku. Itakukuta moja kwammoja hapo ndani, nawe uko hapo. Hakuna njia ya kutoka humo wakati huo; tayari umeipokea. Tokeni!

Malaika alishuka kutoka Mbinguni, akiwa na uso mkuu unaong'aa, na akawalilia watu. Iliitikisa dunia. "Tokeni Babeli, kwa maana imeanguka. Msishiriki mapigo yake, enyi watu Wangu!" Tokeni kwake. Ondokeni! Hivi hatukusoma tu katika Neno, muda mfupi uliopita? Malaika ni "mjumbe," mnaona, akishuka. Angalia Roho Mtakatifu, "Tokeni kwake, msijekuwa washiriki."

94 Sasa yeye amejenga mambo haya yote. Amejenga makanisa makubwa. Amejenga chuo, mashule, akiwachukua watu na kuwaelimisha kufikia, unavyoitwa, ustaarabu bo—bora zaidi. Nao wamewaelimisha kwa ustaarabu wa kisasa uliowaleta kwenye shimo la mauti, kwa maarifa, mbali na Mungu na Neno Lake.

Hivi hamwoni mpango mzima? Mnaona jambo hilo, enyi kanisa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Huko nje hewani, kama mkiona jambo hilo katika makusanyiko yenu wenyewe huko nje, semeni "amina," waliosalia watajua mahali mnaposimama. Mnaona?

Yeye amefanya hivyo. Yeye ni … Ni mungu wa dunia hii, naye amejenga vyuo. Amejenga vyuo vikuu. Amejenga hospitali. Amejenga maktaba. Amejenga vitu hivi vyote kwa ajili ya msaada wa dhararu wa mwanadamu, vya kutosha tu kuwadanganya, kuondoka kwenye hilo Neno. Naye aliwaongoza kwa nini? Ulimwengu wote wa kanisa umetumbukizwa katika mauti, kwa kuwa Mungu alisema ya kwamba angemteketeza yule kahaba, na watoto wake, kwa moto wa milele.

Tokeni kwake, enyi watu! Msishikwe mle ndani. Ondokeni kwenye kitu hicho upesi mwezavyo!

Kwa maarifa yake ya kisayansi, ameweza kufanya jambo hili, sasa angalia, bila Neno la Mungu.

95 Mungu kamwe hakutuagiza tuende na kuwa na shule. Yeye kamwe. Yeye hakutuambia kamwe kujenga hospitali. Hayo ni mema. Yeye hakutuambia kamwe kujenga maktaba. La, bwana. Yeye kamwe.

Yeye alisema, "Ihubiri Injili." Na, Injili, inadhihirisha, ikionyesha nguvu za Roho Mtakatifu.

Paulo alisema, "Injili ilitujia, si kwa neno tu, bali kwa udhihirisho na dhihirisho la Roho Mtakatifu." Paulo alisema, "Sikuja kwenu kwa ufasaha wa maneno ya hekima ya daktari fulani na kadhalika, lakini nilikuja kwenu katika nguvu na dalili za Roho Mtakatifu; ili imani yenu isiwe katika hekima ama maarifa ya watu wa dunia hii, bali katika nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo; kwa sababu Yeye yu hai, yeye yule jana, leo, na hata milele." Mungu na atusaidie kuamini jambo lile lile, na Mungu athibitishe jambo lile lile ambalo amekuwa akifanya.

96 Yeye hukuzuia usione ufunuo wa kweli na imani ya Neno la Mungu likifunuliwa na kuthibitishwa leo, na shule zake, maktaba, fasihi, hospitali, na kadhalika. Mnaona? Yeye hukuzuia. Yeye sasa anafasiri, kama alivyomfanyia Farao, akijaribu kukufanya usione maana ya Neno lililothibitishwa la wakati Wake ulioahidiwa katika Nuru ya jioni, ikithibitishwa na kuhakikishwa. Yeye amejaribu, kwa maarifa yake, na shule, na watu walioelimika vizuri zaidi, na maadili, na kadhalika, kukuzuia usione jambo Hilo.

Chochote, kusudi usiangalie jambo Hilo na uone huyo ni Yesu Kristo! Unajuaje ni Yesu Kristo? Yeye ni Neno, Naye ni Neno la wakati huu. Na wakati huu, alisema ya kwamba jambo hili lingetukia katika wakati huu, na hili hapa linatukia. Mnaona? Mnaona? Yeye akijaribu awezavyo kukuzuia usione jambo Hilo.

Yeye ataweka jina lolote chafu juu Yake awezalo. Mnaona? Yeye ataliita "watakatifu wanaojifingirisha" na chochote kile. Alimwita Yesu "Beelzebuli." "Nao wanamwita Bwana wa nyumba Beelzebuli, ni zaidi sana vipi watawaita wanafunzi?" Mnaona?

97 Mnaona, kujaribu kukuzuia usione maana halisi ya Neno. Si kile … Mnaona, yeye analifasiri Hilo, akisema linamaanisha hivi.

Mungu alisema, "Niliahidi katika siku za mwisho ningewapelekea Malaki 4." Haihitaji kufasiriwa; Yeye alifanya hivyo. Yeye alisema, "Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ulimwengu utakuwa katika hali ya Sodoma; na katika wakati huo, nitamfunua Mwana wa Adamu kwa jambo hilo, hasa." Tuna kila namna ya uigaji na kila kitu kingine, cha jambo hilo, bali tuna Yule halisi, pia. Mnaona? Yeye alisema angefanya hivyo.

Yeye alisema mpinga-Kristo angeinuka na karibu awadanganye Wateule kama yamkini. Lakini alisema, "Waacheni. Acha waendelee. Upumbavu wao utaonekana." Kwa nini? Jaribio la Neno hulithibitisha. Mnaona?

Wakati ilipofikia kwenye Neno hilo, "Hiyo ilikuwa imerudi *hivi*, *vile*? Loo, siamini uzao wa nyoka. Siamini katika *hili, lile*, na *lingine*." Haijafunuliwa kamwe, mnaona, la, kamwe. Loo, ndugu, angalia tu ambapo …

Itatubidi kufunga, kwa sababu ni saa sita.

98 Angalia, anajaribu kukufanya usione maana ya Neno la wakati huu, ya Nuru ya jioni ikifasiriwa. Ni … Inamaanisha nini? Ni wakati wa kutoka umekaribia, Mungu anakuja kwa ajili Yake, hakika kabisa kama ulimwengu. Mnaona?

Sasa nataka kuwaulizeni swali. Wakati, ni saa sita sasa, dakika tano baadaye; nasi tutaendelea, usiku wa leo. Mnaona mungu wa wakati huu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaamini jambo hilo? ["Amina."] Mnaona jinsi ilivyo, kanisa, la kielimu, sayansi?

Ulimwengu mzima ni mali yake, mnaona, madhehebu. Na, unasema, "Mimi ni Mkristo." "Wewe ni wa dhehebu gani?" Vema, kama nilikuwa mfuasi wa dhehebu fulani, siamini ningekuwa Mkristo. Sasa, hilo ni neno kubwa, bali hilo ni kweli.

Nimemaliza tu kusema ya kwamba maarifa na sayansi, na Ukristo, hauna ushirika hata kidogo. Kimoja ni cha ibilisi, na hicho kingine ni cha Mungu. Chochote kinacholikana Neno la Mungu, jiepushe nacho. Mnaona? La, bwana. Biblia inawahimiza Wakristo, kwa siku hizi za mwisho, watoke kwa kahaba huyo, huo ni mti wa kujua mema na mabaya.

99 Hakika, yeye ana mema. Je! Mtu ye yote anaweza kusema mabaya juu ya hospitali? La, bwana. Maktaba? La, bwana. Elimu? La, bwana. Lakini, mnaona, wanawapa hiyo bila Neno. Mnaona jinsi lilivyo la udanganyifu? Akiwapa kanisa la kwenda, ibada ya kuabudu, "mungu anayeketi juu ya kiti cha enzi." Biblia ilitabiri jambo hilo.

Sasa wewe ni mfuasi wa moja ya mashirika hayo. Kuna mawili tu ya hayo duniani sasa, daima imekuwa hivyo, na itakuwa hivyo mpaka Yesu atakapokuja, na moja ya hayo litaharibiwa. Sasa wewe ni mfuasi wa moja ya makundi hayo. Mmoja wao, umejiunga naye; huyo mwingine, umezaliwa ndani Yake. Mnaona?

Mmoja wao, wewe ni sehemu yake kwa sababu umezaliwa ndani Yake. Huna budi kuwa sehemu Yake. Ningeweza kukana kwamba nina mkono? Si zaidi ya vile ninavyoweza kukana Neno lo lote la Mungu, kama mimi ni sehemu ya Mungu. Mimi ni sehemu ya William Branham; Mimi niko katika sehemu, na kila sehemu ni sehemu yangu. Na kila Neno la Mungu halina budi kutosheleza roho yangu, halina budi kutoshea nafsi yangu, halina budi kutoshea maisha yangu, Hilo linapaswa kutoshea mawazo yangu. Kama mawazo yangu ni kinyume na Hilo, basi Roho wa Mungu haishi ndani yangu. Hiyo ni kweli. Huwezi kukana Neno moja Lake.

100 Wewe ni mfuasi wa mmoja wa makundi hayo. Haina budi kuwa, haina budi kuwa. Ama ni Mwili wa Mungu, ambao uko kwa Neno; ama mwili wa Shetani, kwa kanisa. Na ulimwengu wote itawabidi kuwa wafuasi wa kanisa fulani; unamwabudu mungu fulani. Huna budi kuabudu aidha mungu wa maarifa,

unategemea yale unayosikia kwa maarifa, unatemeagea *hili*, ama *lile*, ama *lingine*; ama unategemea Neno la Mungu, kwa imani, ukimtarajia Yeye alithibitishe na kulifanya kweli.

Kanisa halisi la Mungu linatazamia kuja kwa siku hiyo yenye furaha ya Utawala wa Miaka Elfu,
Wakati Bwana wetu aliyebarikiwa atakapokuja na kumnyakua Bibi-arusi Wake anayengojea;
Loo, moyo wangu umejawa na kunyakuliwa ninapofanya kazi, kukesha na kuomba,
Kwa kuwa Bwana wetu anarudi duniani tena.
Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa na mjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

101 Loo, enyi watu wa Marekani hii, ambako Ujumbe huu unaenda sasa, kimbieni sana mwezavyo na maarifa haya, wakati wa kisayansi tunaoishi. Likimbilieni Neno la Mungu!

Ninyi, mimi, hakuna mtu ana—anayeweza kuthibitisha jambo Hilo; Hakuna mtu awezaye kulihakikisha Hilo. Mungu hufanya uthibitisho Wake Mwenyewe. Hakuna mtu aliye na haki ya kulifasiri; mimi, hakuna mtu mwingine aliye na haki. Mungu hujifasiria Mwenyewe. Yeye alitoa ahadi. Yeye alisema angefanya jambo hili katika siku za mwisho.

Na katika siku za mwisho mungu wa wakati huu mwovu angeyapofusha macho ya watu, kwa maarifa yake ya kiakili, juu ya mti uliochanganyikana wa mema na mabaya, akiwa bado anawapa watu hayo. Na hapa inakuja, jambo hilo likiendelea, madhehebu hayo kutoka huko nyuma kabisa katika Nyakati za Giza, na kabla ya Nyakati za Giza, yote yakiishia kwenye mtu maalum, Shetani, aliyesema, "Nitajiinua nafsi yangu juu ya wana wa Mungu, nao watanisikiliza." "Naye kama Mungu ataketi katika hekalu la Mungu, nao wana wa Mungu watalipenda sana."

102 Mbona, mwana wa Mungu, aseme, "Vema, mke wangu, sivyo; yeye ni mzuri …" Endelea, endelea tu. Mnaona?

Mnasema, "Vema, Yeye alisema 'wana wa Mungu.'" Naam, bwana.

Mwanadamu, ye yote yule, aliumbwa kwa mfano wa Mungu, kwa utukufu wa Mungu. Na mwanamke ni kitu kilichotoka kwa mwanamume, si cha Mungu. Sawa. "Wakati wana wa Mungu walipoona binti za wanadamu ni wazuri, wakajitwalia wanawake."

"Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

Sasa angalia, ukitaka kujua kanisa liko kwenye kiwango kipi, angalia wanawake wako kwenye kiwango kipi, mnaona, maana mwanamke ni kanisa. Angalia kile anachofanya, mnaona, na katika wakati huu mwovu.

Angalieni, hapakuwapo na mji wa kinyama, mwovu, wa chini, na ukahaba ulimwenguni, kuliko Nazareti, na kutoka humo Mungu alimchagua bikira. "Kuna kitu chema kinachoweza kutoka Nazareti?"

Na kutoka katika wakati huu mwovu, ambapo mungu wa wakati huu amepofusha macho ya watu, kwa mafundisho yao ya sharti na madhehebu; Kutoka kwenye wakati huo, Mungu anachagua watu kwa ajili ya Jina Lake.

Ingawa hapa wametelekezwa na kudharauliwa, siku moja Bwana atawaleta
Wateule Wake ndani ya lango, na hilo linastahili kila kitu.
Ndipo tutaimba na kupaza sauti, na kucheza,
Mwana-Kondoo atayafuta machozi yetu;
Tutakuwa na juma moja la kurudi nyumbani kwa furaha,
Miaka elfu kumi ya kwanza. (Hiyo ni kweli.)
Watu wa ajabu kwa Jina Lake nao wanaitwa Bibi-arusi Wake. (Hiyo ni kweli?)
Ingawa wametelekezwa na kudharauliwa, siku moja Bwana atawaleta
Hao waliochaguliwa ndani ya lango, (katika kutoka) na hilo lina thamani ya kila kitu kwangu.

103 Ninakuwa mzee. Na siku zangu zinaanza kwisha; na macho yangu yanaanza kufifia; na mwali wangu wa maisha unaanza kufifia. Siogopi giza. Kwa kuwa ninataka kusema jambo hili, pamoja na Paulo, "Ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake." Haidhuru watanizika wapi, kama nikizama baharini, ama nikiteketea katika tanuru, au nikiliwa na simba, Yeye ataliita jina langu, nami nitanena. Amina!

Hebu na tuombe.

Kama yupo hapa, ama huko nje kwenye simu za huu Ujumbe kila mahali nchini, katika makanisa yenu madogo na makundi na kwenye kumbi, na po pote mnapoketi, kama kuna mmoja, loo! hebu nikushawishi; hebu nikusihi, kama mhudumu wa Injili; hebu nikusihi, katika Jina la Yesu Kristo; itoroke hasira ya wakati

huu mwovu! Usimtumikie mungu wa wakati huu mwovu. Usimtumikie mungu wa wakati huu mwovu.

Loo, ninajua mnasema, "Ni vizuri. Ni wazuri." Hakika, mti uliochanganyikana. Huwezi kuchanganya maarifa na Neno la Mungu.

Ni Neno linalopaswa kuaminiwa kwa imani, si maarifa. Hulifahamu; unalikubali. Unasema ni kweli, halafu unaishi kwalo. Hayo ndiyo tu anayokuomba ufanye.

Kama kuna ye yote aliyeko hapa katika kikundi chetu, hatuwezi kufanya mstari wa maombi kuwaleta hapa, kwa maana hakuna nafasi; ama huko nje hewani, huko kwenye simu, kama kuna mtu huko asiyemjua Yeye. Msininii …

104 Loo, enyi wanawake, nimewakemea asubuhi ya leo, si mimi, nimenukuu tu Neno. Nywele fupi, kuvaa maskini hizo nguo fupi, kuvaa uonekane kizinifu kweli kweli, hivi hutambui ya kwamba roho huyo ambaye… Huenda ukawa msafi, dada, mpendwa, linapofikia mwili wako, lakini katika nafsi yako huoni kilichokushika?

Je! Mungu angemfanya binti Yake aonekane mchafu kumdanganya mwanawe, kumtamani, kuwafanya wote wawili kuwajibika kwa uzinzi? Angefanya hivyo, dada? Jiulize swali hilo. La, si kwa maili milioni kumi. Usiweke hilo kwa Mungu.

Ndugu, hivi mungu amekupa roho ya ulimwengu huu hata huwezi kuona ya kwamba hilo ni kosa? Hivi yeye amepofusha macho yako, kwa maadili ya kanisa, madhehebu, kanuni za imani, na kadhalika, hata huwezi kuona ya kwamba Mungu anathibitisha Neno Lake na kulifanya ni kweli Hivi kazi yako, tajiri wako, mke wako, watoto wako, kanisa lako, ama cho chote, vimekutenganisha na Neno la Mungu, ambalo ndilo chanzo pekee cha Uzima? Ikimbie, ndugu yangu! Ninawapenda, kwa upendo wa kiungu. Mimi siheshimu ye yote wa ndugu zangu zaidi yako, hata kidogo. Kama ningefanya hivyo, ningeonyesha heshima kwa mtu. Sisemi mambo haya kukufanya uwe na hasira. Ninaonyesha, ninasema mambo haya kwa sababu yako katika Neno la Mungu. Na kama mtumishi wa Mungu, na upendo wa Mungu moyoni mwangu, ninawaambia mambo hayo ili mpate kuona na kufahamu. Labda usingejua kama sikukuambia. Mtaikimbia leo?

Sasa, kila mahali kote nchini, hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

105 Mungu mpenzi, zilizowekwa mbele yangu ni leso. Watu ni wagonjwa; Ninaweka mikono yangu juu yao, ili kwamba utawaponya.

Nami ninatumaini, Bwana, usiku wa leo, ya kwamba kutakuwako na ibada kuu, ya kwamba Nguvu za Mungu zitakuwa hapa, ishara kuu na maajabu. Tuliposikia matokeo kutoka kwenye mikutano hii michache iliyopita, jinsi yalivyo makuu sana, angalia kile kilichotukia! Ninaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba utatupa sehemu maradufu usiku wa leo. Ninaomba kwa moyo mnyofu, Bwana, kwa sababu ni upendo wangu Kwako na kwa Neno Lako, na kwa ajili ya watu hawa. Tujalie, Mungu mpendwa.

Na kama huko nje kote nchini, ama hata humu ndani sasa, kwamba kuna wengine walio wagonjwa na wanaoteseka, na hawana budi kuondoka usiku wa leo, hawatakuwa hapa, ama watakuwa huko nje makanisani ama mahali wanapokutana; Ninaomba Wewe uwaponye. Sasa, Bwana, lakini kwa uponyaji mkuu kuliko wote! Kama ukiponya miili yao ya kimwili kutokana na kansa, TB, nimonia, kitu fulani, watakuwa wagonjwa tena, hapana shaka, kama wakiishi muda mrefu sana, kwa kuwa miili yao ingali chini ya dhambi, laana. Lakini hebu wapate u—uponyaji halisi wa Kiungu, uponyaji wa nafsi, ambao unawafanya kiumbe kipya, unapita kutoka mautini kuingia Uzimani, halafu unangojea katika maskani hii ya kale ukombozi wa mwili baada ya nafsi kukombolewa. Tujalie, Bwana.

Jalia wakimbie hayo madhehebu na kanuni za imani. Mungu, huko nje kabisa katika hizo kanuni za imani na madhehebu nimekutana na baadhi ya ndugu wazuri sana. Na, Mungu, ninawezaje kusema jambo hilo kwamba wataona, na kuwaacha walione Neno? Inanisumbua. Lakini ninajua, tena, ya kwamba Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja," haidhuru ni mwema namna gani, namna alivyo mpole, namna alivyo mpole, "isipokuwa Baba Yangu amwite. Na wote alionipa Baba Yangu, watakuja." Na, Bwana, ninajisikia wajibu wangu pekee wa kusema Kweli.

Na si kama alivyosema Paulo, "Kulichanganya Neno la Mungu na uongo," pamoja na mafundisho ya sharti ya madhehebu yamechanganywa ndani Yake, kama mti wa mchanganyiko wa mema na maarifa, mema na mabaya; bali tukiwa na moyo mkunjufu pamoja na Roho Mtakatifu. Tujalie, Mungu. Okoa kila mmoja.

106 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa na macho yetu yamefumbwa. Na si kwangu mimi … Siwezi kulisema hivi, "Haileti tofauti kwangu kama unafanya au la." Haileti tofauti. Ninawapenda. Nami natumaini hamfikirii kwa sababu inanibidi kuzungumza kwa ukali … Kama vile Paulo alivyosema, "Ningekuwapo pamoja nanyi sasa, ningebadilisha msimamo wangu." Si kwa sababu hakuwapenda; aliwapenda. Si … Kama vile ilimbidi Yesu kuwakemea, kisha akawafia. Mnaona, "Baba, wasamehe; hata hawajui wanachofanya." Kuwazia, binadamu anayetaka kuwa sahihi, na kujaribu kuwa sahihi, na kumwona yule

ibilisi… Huyo ndiye ninayempinga, ambaye ameyapofusha macho ya watu hawa.

107 Taifa hili linapaswa kuwaka moto kwa utukufu wa Mungu, kuona kile kilichotukia ndani yake katika siku hii ya mwisho, hii ya mwisho. Kwa nini ufufuo huu haujagusa nchi za kale? Hii ni Pwani ya Magharibi huku, magharibi ya mbali sana uwezayo kwenda. Sasa kizuizi cha dhambi kimenguruma chini ya dunia, nayo inazama; mahali, na Los Angeles na Hollywood, inazama inchi kadha kwa saa, hakuna njia ya kuzuia jambo hilo. Naam, tuko hapa. Karibu wakati wo wote tutasikia wito. Kama unajua ya kwamba …

Sasa, mtu yeyote asiangalie. Lakini kama unajua, kutoka moyoni mwako … Ninawauliza. Siwezi kuujua moyo wako, isipokuwa Mungu aufunue. Lakini kutoka moyoni mwako, kama unaweza kuona ya kwamba hauko mahali unapopaswa kuwa pamoja na Mungu na Neno Lake, katika imani, hebu wewe mwinulie tu mkono wako Kwake, umwambie, "Bwana, nisaidie." Ee Mungu! Kutoka kwenye kanisa hili, limejaa, limejaa kuzunguka kuta, ndani na nje, mamia ya mikono, labda mikono mia mbili iliyoinuliwa. Asante kwa uaminifu wako.

108 Mpendwa Yesu, usiache mmoja wao apotee. Kama mtumishi Wako, anayesimama kati ya walio hai na wafu, akiwaelekeza, kwa kidole, kwenye Neno la Mungu. Siwezi kuwaokoa, Bwana, bali wanataka kuokolewa. Na, Baba, kama nilivyosema mara nyingi, jua huchomoza asubuhi; na inapokuja kote duniani, limetumwa na Mungu kuivisha nafaka, kutengeneza chakula cha kawaida kwa maisha ya kawaida. Lakini, Ee Mungu, Wewe ulisema, "Kwa wale wanaolicha Jina Lake Jua la haki litawazukia likiwa na uponyaji katika mbawa Zake." Jalia Jua la haki, Neno la Mungu, lizuke katika mioyo ya watu, na miale ya uponyaji ya imani katika Neno hilo inamponya kila asiyetii Neno, na kuwaleta kwenye utimilifu wa wana na binti za Mungu.

Wao ni Wako, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, hapa na nje hewani, ninawakabidhi hao walioinua mikono yao Kwako kwa ajili ya wokovu wa nafsi zao. Amina.

Hapo nafsi yangu itakayokuliwa itakapopata (Wapi? Kwenye madhabahu hii.)
Pumziko ng'ambo … (kwa imani ninaangalia kule ninakoelekea)
Karibu na msalaba, (hapo ndipo Neno linaponing'inia) … msalaba,
Iwe utukufu wangu daima;
Mpaka nafsi yangu itakayonyakuliwa itakapopata
Pumzika ng'ambo ya mto.
Yesu, nidumishe … (Hiyo ni kusema, kusulubiwa pamoja Naye, sitaki kitu cho chote cha ulimwengu. "Niweke msalabani.")
Kuna chemchemi ya thamani,
Ni bure kwa wote, kijito cha uponyaji,
Inatiririka kutoka kwenye chemchemi ya Kalvari.
Msalaba, msalaba,
Uwe utukufu wangu (hebu tuinue mikono yetu) daima;
Mpaka nafsi yangu itakayonyakuliwa itakapopata
Pumzika ng'ambo ya mto.

109 [Ndugu Branham sasa anazungumza na wanamuziki — Mh.] "Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita."

Nyosha mkono na ushike mkono wa mtu fulani, na useme, "Mungu akubariki, Mkristo."

[Ndugu Branham anazungumza tena na wanamuziki — Mh.] "Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita."

Mnahisi Uwepo Wake? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Huko nje juu ya mawimbi ya simu, nyote mnapeana mikono huko nje, na kusema, "Mungu akubariki, Mkristo."

110 Mnajua, kuna kidimbwi cha maji nyuma hapa. Yeye anawachukua watu waliovaa Jina Lake. Hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako, kuna kidimbwi, kuna majoho, kuna mtu anayesimama tayari. Unakaribishwa, kama kweli unamkubali Yesu kama Mwokozi wako na unaamini ya kwamba hiyo ni Kweli.

Kumbukeni, hakukuwa na mtu katika Biblia, wala wakati wo wote kabla ya kuanzishwa kwa kanisa Katoliki, aliyewahi kubatizwa kwa njia nyingine yo yote ila katika Jina la Yesu Kristo. Hakuna mahali panapopatikana katika Maandiko, au historia, ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa, katika Kanisa la Mungu aliye hai, katika jina la vyeo vya "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ni fundisho la sharti la Katoliki, wala si fundisho la Biblia.

111 Nilipokuwa nikihojiwa na kasisi fulani, nilimwuliza hivyo. Yeye alisema, "Hiyo ni kweli. Lakini sisi ni kanisa; tunaweza kubadilisha chochote tunachotaka. Uchaji uko katika kanisa. Mungu yuko katika kanisa Lake."

Nikasema, "Mungu yuko katika Neno Lake. Na kama kanisa ni …" Nikasema, "Mungu ni Neno. Na kama kanisa linapingana na Neno, basi siamini kanisa."

Ninaacha kila neno la mwanadamu liwe uongo, kama ni kuhani, papa, chochote kile, na Neno la Mungu liwe kweli.

Naye Paulo alimfanya kila mtu, haidhuru alikuwa amebatizwaje, kama hakubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, aje abatizwe tena.

Na baada ya wengine kumpokea Roho Mtakatifu, Petro alisema, "Je! Tunaweza kukataza maji, kwa kuwa hawa wamempokea Roho Mtakatifu," Matendo 10:49, "kwa kuwa hawa wamempokea Roho Mtakatifu kama tulivyompokea …" Naye akawaamuru, "Kabla hamjaondoka mahali hapo, ingawa mmempokea Roho Mtakatifu, njoni mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo."

Kwa kuwa, Petro alipewa ufunguo wa Ufalme, akisema, "Lolote mtakalofunga duniani, nitalifunga Mbinguni." Na ufunguo hufanya nini? Unafungua kitu fulani, ile siri.

112 Na wakati Yesu aliposema, "Enendeni, mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," akiweka hayo pale kumpofusha asiyeamini.

Angalia! Kwa nini Petro hakutekeleza hilo, neno kwa neno? Ilimbidi.

Kama mtu amebatizwa katika vyeo, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," yeye hajabatizwa kamwe; hana Jina. Baba si jina, Mwana si jina, na Roho Mtakatifu si jina. Roho Mtakatifu ndivyo alivyo; kama, mimi ni mwanadamu. Ni Roho Mtakatifu.

Baba ni cheo; Mimi ni baba. Mwana ni cheo; Mimi ni mwana. Mwanadamu ni cheo; hivyo ndivyo nilivyo. Lakini jina langu ni William Branham.

Na Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu ni Jina la "Yesu Kristo." Yesu alisema, "Nimekuja katika Jina la Baba Yangu." Jina la Baba ni lipi? Mwana yeyote huja katika jina la baba yake. Na Jina la Baba ni Yesu Kristo. Mnaona? Mnaona ninalomaanisha?

113 Kama niliwaambia mshuke mniletee kitu fulani kutoka kwenye kaunta hapa chini, katika jina la meya wa jiji. Ni wangapi wanaojua meya wa jiji hili ni nani? Rafiki yangu mzuri, Rich Vissing. Vema, usingeenda huko chini na kusema "kwa jina la meya wa jiji." Mnasema, "Katika jina la Richard Vissing." Ninyi watu hapa Jeffersonville mnajua yeye ni nani.

Na hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Ndani Yake mnaishi Uungu, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye alisema, "Wabatizeni katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu."

Petro akiwa amesimama pale akiwa na ufunuo ambao Yeye alijenga Kanisa, juu ya kwamba Yeye alikuwa nani, alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Na kamwe … Funguo zilizungushwa Mbinguni na duniani. "Hakuna Jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu litupasalo kuokolewa kwalo."

114 Kwa nini unabatiza katika Jina la Yesu Kristo? Kwa ajili ya ondoleo la dhambi. "Kila mtakayemwondolea dhambi, zimeondolewa." Mnaona? Lakini kama hufikiri yeye anastahili na anastahili kubatizwa, usifanye hivyo. Kwa kuwa, unapofanya jambo hilo, hilo linafanyu hivyo, mnaona. Mnapata kile ninachomaanisha?

Ninaweza kumsikia Mwo-…(Neno) akiita, (akiita kule chini kaburini)
Ninaweza … ("Je! Hamtakufa pamoja na Mimi, ili mweze kufufuka pamoja Nami?") … -
Kuitwa kwako,
Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita, (ulimwengu utasema nini?)
"Chukua msalaba wako, ufuate, ufuate …"

Sasa, kama hujaninii:

Ambapo Yeye (Yeye ni Neno) huniongoza mimi … (hapo pana kidimbwi)
Aniongozako nitafuata,
Aniongozako nitafuata,
Nitaambatana Naye, pamoja Naye njia nzima.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

115 Mungu mpenzi, kidimbwi kiko tayari. Sasa nena na mioyo, Bwana. Jalia wamsikie Kristo, Neno, akiwaita, na waende pamoja Naye njia nzima.

"Nitaenda pamoja Naye bustanini. Nitaenda pamoja Naye kwenye kidimbwi. Nitachukua Jina Lake. Ninataka kuwa mmoja wa watu anaowaita kwa Jina Lake. Nitaamini Neno Lake. Nitafuata. Sitabembana na ulimwengu kamwe. Nitakuwa Bibi-arusi wa kweli, aliyeposwa. Sitaacha hata sehemu moja ya Neno

Lake. Kila ombi, nitakuwa Bibi-arusi halisi, wa kweli. Kila kitu anachoomba nifanye, hicho nitafanya.

"Kama Mume wangu anayekuja anataka niachilie nywele zangu, nitafanya hivyo. Kama Yeye ananitaka niondoe vipodozi hivi vyote, nitafanya hivyo. Kama akitaka … Yeye ananiambia ni pepo mchafu, yule mwovu ninayembembana naye, na nguo hizi zinazoonekana ni za kizinifu; Nitafanya hivyo, nitaziondoa. Sijali yale mtu mwingine ye yote asemayo, nitaziondoa.

"Ananitaka nitoke kwenye kundi hilo nililo nalo, la wasioamini, nitafanya hivyo; ingawa ninaoka mkate wangu, ama cho chote kile. Yeye aliahidi hataniacha kamwe wala kunipungukia. Nita—nitafanya hivyo. Nitaambatana Naye kote. Ananitaka nibatizwe katika Jina Lake, nitafanya hivyo."

Bwana, Wewe uliahidi jambo hilo katika Neno Lako hapa, hilo ndilo ulilotaka. Bwana, Wewe uliahidi jambo hilo katika Neno Lako hapa, hivyo ndivyo ulivyotaka. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

116 Ninyi ni wa Mungu. Mungu na ayachukue maneno hayo madogo yaliyovunjika na kuyafanya halisi kwako, ndilo ombi langu nyofu.

Kidimbwi kitakuwa tayari. Mtu yeyote anayetaka kuja, wana … Mhudumu atatangaza hilo baadaye kidogo. Mtu yeyote ambaye ametubu na anataka kubatizwa, kwa kutumia Jina la Yesu Kristo, wewe njoo moja kwa moja. Kila kitu kiko tayari. "Mambo yote yako tayari." Kila kitu tunachoweza kufanya kukusaidia kumwishia Mungu, tuko hapa kukifanya. Mungu akubariki.

Sasa hebu na tusimame. Sasa wimbo wetu mdogo, Nampenda. "Nampenda sababu alinipenda." Hebu na tuuimbe, kila mtu sasa.

Nampenda, …

Hebu na tuinue mikono yetu tunapouimba.

… Nampenda<br>
Sababu alinipenda<br>
Na kununua wokovu wangu<br>
Mtini kwa Kalvari.

Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa sasa, hebu na tuuvumishe kwake. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha Nampenda — Mh.]

Ninampenda.

[Ndugu Branham anaendelea kuvumisha *Nampenda — Mh.*]

Ee Mungu, Baba yetu, uturehemu sisi viumbe duni, Bwana. Tutie nguvu kwa ajili ya kazi iliyo mbele yetu. Nisaidie, Ewe Mungu, nisaidie! Ninajisikia ya kwamba kitu fulani kiko papa hapa nje, Baba. Nisaidie, Ewe Mungu, kujua ile Kweli. Wabariki watu hawa, Mungu mpendwa. Waongoze, ninaomba, katika Jina la Yesu.

Sasa wakati tunapoinamisha vichwa vyetu, nitamwomba mchungaji hapa, Ndugu Neville, ndugu yetu wa thamani, aje moja kwa moja hapa sasa na kusema kile atakachoenda kusema, kuhusu kama … kuhusu ubatizo. Huenda nikatangaza jambo hilo. Nafikiri kidimbwi kiko wazi, hata hivyo.

MESSAGE hub online

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info